

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tisa - Tarehe 12 Novemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wa Tano na leo ndiyo siku ya mwisho ya Mkutano wa Tano kwa maana ya Kikao cha Tisa. Katibu!

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero.

Na. 89

Ahadi ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya – Kilombero

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mhe. Waziri Mkuu aliyoitoa mwaka 2018 ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kilombero?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Dugange, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri nchini kote. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali 102 na kuanza ujenzi wa hospitali mpya kwenye halmashauri 28 zikiwemo hospitali zilizoahidiwa na viongozi wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Ifakara ni mionganoni mwa halmashauri 28 zisizo na Hospitali za Halmashauri, ambayo imetengewa fedha shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo matatu ya awali. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Asenga.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, napenda kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya kutekeza ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu maana Waziri Mkuu mwenyewe alilitembelea eneo hili na aliona ufinyu wa eneo hili. Napenda pia kuishukuru Serikali kwa Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi kutupatia ardhi Kata ya Kiberege kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hii ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa sasa hivi wakati mchakato wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ukiendelea Wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara wanategemea sana kituo cha afya cha Kibaoni, kituo hiki kinakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi.

Je, Serikali haioni kuchukua hatua za haraka kuongeza watumishi katika kituo cha afya cha Kibaoni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kutokana na ufinyu wa ardhi na eneo la ekari takribani kumi za kujenga Kituo cha Afya cha Kata ya Ifakara Mjini, Ifakara Mjini mpaka sasa hivi haina Kituo cha Afya eneo lilitopo ni dogo. Je, Serikali ipo tayari kutupatia ramani maalumu ya ujenzi wa ghorofa ili tufanye mchakato wa kuanza Kituo cha Afya cha Kata ya Ifakara Mjini?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa DKt. Festo John Dugange, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee shukrani zake nydingi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi ambayo imeendelea kuifanya ya kujenga vituo vya afya, hospitali na zahanati nchini kote na nimuhakikishie kwamba mpango huo ni endelevu tutaendelea kujenga vituo vya afya, zahanati, lakini na hospitali zetu za halmashauri kuhakikisha tunasogezza huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kituo cha afya cha Kibaoni kuwa na watumishi wachache nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa vituo hivi unakwenda sambamba na mipango ya kuajiri watumishi kwa awamu kwa kadri fedha zitakapopatikana, lakini pia kwa kadri ya vibali vya ajira vitakavyotolewa. Kwa hiyo, naomba nichukue suala hilo na tutakipa kipaumbele kituo cha afya cha Kibaoni ili kiweze kupata wahudumu kwenye awamu za ajira zinazofuata ili tutoe huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kituo cha afya Ifakara Mjini utaratibu upo wazi kama tunahitaji kujenga jengo la kwenda juu kwa maana ya ghorofa. Tunaomba kibali rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunawasilisha michoro na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuititia watalaaamu tunapitia na kuwashauri namna ya kujenga. Kwa hiyo tunakukaribisha kuwasilisha maombi hayo ili tuweze kuona uwezekano wa kujenga kituo hicho. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Nimekuona Dkt. Ishengoma uliza swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kituo cha Afya cha Mwaya – Mahenge – Ulanga majengo yake yamejengwa kwa muda mrefu na ni mabovu. Je, ni lini kitafanyiwa ukaratibu Kituo cha Afya hiki cha Mwaya? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Dugange tupo kwako bado.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vyetu na hospitali zote za halmashauri chakavu ambazo zimejengwa muda mrefu zinaandaliiwa utaratibu wa kwenda kuzifanyia ukarabati. Kwa hivyo tumeshaanza na utaratibu wa hospitali za halmashauri, tumeshazitambua hospitali 23 kongwe, lakini tutakwenda kutambua vituo afya chakavu vya siku nyingi ili tutafute fedha kwa awamu kwa ajili ya kuvifanyia ukarabati, lakini pia kuvifanyia upanuzi wa vituo vile. Kwa hiyo, naomba nimuhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati zoezi hilo linafanyika tutahakikisha pia Kituo cha Afya cha Maya kinapitiwa na kufanyiwa tathimini hiyo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata uliza swali lako.

Na. 90

Ujenzi wa Barabara ya *Kalambo Falls*

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka *Kalambo Falls* hadi barabara kuu inayokwenda Matai yenyе urefu wa kilometra 17?

SPIKA: Majibu ya Serikali kwa swali hilo Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ukarabati wa barabara hiyo yenyе urefu wa kilometra 17 kwa kiwango cha Changarawe unaendelea ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) kwa Halmashauri ya Wilaya Kalambo kwa kushirikana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kwa maana ya *TFS* ulitumia kiasi cha shilingi milioni 139.72 kukarabati sehemu ya barabara hiyo kipande chenye urefu wa Kilometra 10.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) Halmashauri ya Wilaya Kalambo umetenga kiasi cha shilingi milioni 84.5 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum kwa maana *Periodic Maintenance* kipande chenye urefu wa kilometra 4 na Mkandarasi amekwisha patikana na yupo eneo la mradi akiendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara hii kwa sasa inaridhisha kwani inapitika katika kipindi chote cha mwaka. Aidha, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo yake kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Bupe.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru sana, kwanza naipongeza Serikali kwa kazi inayoondelea, lakini pia nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maporomoko haya ya Kalambo Falls ni kivutio kikubwa sana kwa Mkoa wa Rukwa, sasa Serikali ina mpango gani wa kujenga lami kwa sababu wawekezaji na watalii wanapenda sana vitu vizuri kama lami, vitu vizuri kama umeme. Sasa Serikali ina mpango gani wa kutengeneza miundombinu kwenye maporomoko hayo? Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Silinde, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hili aliloliletta Mheshimiwa Mbunge ni ombi kwa sababu ya umuhimu mkubwa wa maeneo haya ya maporomoko ya *Kalambo Falls*. Kwa hiyo na sisi tuseme tu kwamba tumelipokea tutafanya tathimini na tutaangalia mfuko wetu jinsi ulivyo kama fedha itapatikana basi tutailekeza Ofisi ya Rais kuitia *TARURA* Kalambo waweze kwenda kujenga huko. Lakini kwa sasa tutakwenda kufanya tathimini halafu tuone jinsi tutakavyopata fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami katika eneo hilo. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

Na. 91

Mgogoro wa Ardhi Kati ya Wanakijiji na Gereza la Namajani

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza amri ya Mahakama ya kuwalipa fidia Wanakijiji wanaozunguka katika eneo la Gereza la Namajani?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Napenda Kujibu Swali La Mheshimiwa David Cecil Mwambe Mbunge wa Jimbo la Ndanda lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwepo na mgogoro wa ardhi baina ya Gereza la Namajani na wanakijiji wa Kijiji cha Ngalole. Mgogoro huo ultatuliwa na Mahakama kwa kuamuru Jeshi la Magereza kulipa fidia ya shilingi bilioni 2.4 kwa eneo la ukubwa wa ekari 2,064 lilitokuwa na mgogoro.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza amri ya Mahakama ya kulipa fidia kwa wanakijiji wanaozunguka eneo la Gereza Namajani, Serikali kwa nia thabiti tayari imefanya utambuzi wa Wanakijiji wanaostahili kulipwa fidia kama hatua za awali na hivi sasa inaendelea na mchakato wa upatikanaji wa fedha za kulipa fidia hiyo na pindi fedha itakapopatikana italipwa haraka kwa wananchi hao.

SPIKA: Mheshimiwa Mwambe nimekuona.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, majibu haya yaliyoletwa haya *reflect* kabisa hali halisi iliyoko Jimboni Ndanda na Kwenye Kijiji cha Namajani hasa zaidi kwenye Vijiji wa Ngalole, Namajani, Kijiji cha Pangani na Matutwe pamoja na Mahinga.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka swalii hili nilileta kwa mara ya kwanza 2016 na majibu yaliyotolewa yanafanana na kesi hii wanakijiji hawa walishinda mahakamani mwaka 2012 na mara nyingi wizara wamekuwa wanajitetea kwa kusema kwamba wanafanya tathimini na wanatafuta pesa. Kwa mara ya mwisho wamefanya tathimini mwaka jana kabla hatujaingia kwenye bajeti kuu na hakuna pesa yoyote iliyotengwa na Serikali kwa nia ya kwenda kuwalipa kwa hiyo nina amini hawana nia njema sana ili kulimaliza jambo hili. Mgogoro uliopo sasa ni wa malipo.

Sasa swalii langu kama Serikali au Magereza wameshindwa kulipa fedha hii hawaoni sasa kuna haja ya *ku-vacate* na kuondoka eneo hili wakawaachia wananchi wafanye shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili kwa sababu imekuwa ni muda mrefu sana endapo Mheshimiwa Waziri sasa atoe *commitment* kwamba kufikia lini jambo hili litakuwa limekwisha na wananchi wale watakwenda kupata stahiki zao. Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali haya mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe Mbunge Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka tu tuone namna ambavyo tunaweza tukaondoka hapa katika eneo hili, lakini nimwambie tu kwamba waliokuwepo hapa ni chombo cha Serikali ambacho kwa kusema tu tuondoke

tu kirahisi rahisi nimwambie hili kwamba ni jema lakini inabidi sasa tukae tuone namna itakavyowezekana kwa sababu waliokuwepo hapa ni Jeshi na wanashughulikia wananchi na wanasaidia kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini Je, lini hili jambo litakwisha akisoma katika jibu langu la msingi ni kwamba Tayari tumeshaanza hatua kwanza za uhakiki kujua nani anastahili kulipwa na nani hastahili kulipwa zaidi ukizingatia kwamba mahakama amri hapa mahali sisi tuondoke. Kikubwa ni kwamba tunaenda kutafuta fedha kwa sababu hizi fedha siyo kidogo ili tuweze kuwa *compensate* hawa waliokuwepo basi tuone namna itakavyowezekana, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko tafadhali.

Na. 92

Vitendo vya Ukatili kwa Watoto Nchini

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:

Ukatili kwa watoto umekithiri nchini kama vile ubakaji, ulawiti, kuchomwa moto na mimba za utotonii.

(a) Je ni watoto wangapi wamefanyiwa ukatili huo kwa jinsia zao wa kike na wa kiume?

(b) Je kuna takwimu halisi ya hatua zilizo chukuliwa na Serikali dhidi ya matukio hayo nchini?

SPIKA: Bado tuko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri Hamza Khamis tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther

Nicholas Matiko Mbunge Viti Maalum lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia Januari hadi Septemba 2021 takwimu ya vitendo vya ukatili kwa watoto vilivyoripotiwa Vituo vya Polisi inaonyesha jumla ya watoto 6,168 wamefanyiwa ukatili na kati yao wanawake 5,287 na wanaume 881, waliobakwa ni 3,524, waliolawitiwa ni 637 kati yao wanaume 567 na wanawake 70, waliochomwa moto ni 130 kati yao wanaume 33 na wanawake 97, waliopata mimba ni 1,877.

Mheshimiwa Spika, kesi na watuhumiwa waliokamatwa na kufikishwa Mahakamani ni 3,800, kesi zilizo chini ya upelelezi ni 2,368 na kesi zilizohukumiwa ni 88 na nyingine ziko kwenye hatua mbalimbali Mahakamani. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza kwanza kwa takwimu tu za Serikali inaonyesha ni kwa jinsi gani ukatili dhidi ya watoto ni mkubwa sana kwenye nchi yetu ya Tanzania ambayo inaenda kinyume na mkataba wa kimataifa ambao tumeingia wa haki za watoto.

Mheshimiwa Spika, takwimu ambayo Serikali imetoa ni za kuanzia januari tu mpaka Septemba, 2021. Sasa asikwambie mtu kama angetoa uanzia za miaka mitatu au minne nyuma inamaana ni janga kubwa sana na hii inaonyesha dhahiri kwamba kuna changamoto ya uratibu ya takwimu maana hapo umetoa sources moja tu kutoka polisi wakati najua kuna sehemu kama Kamati MTAKUWWA, ukienda kwenye ustawi wa jamii, ukienda kwenye mashirika ya siyo ya Kiserikali lakini hata zile familia ambazo zinamalizana juu kwa juu ukikusanya haya matukio mengi takwimu ni kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninataka kujua ni utaratibu gani Serikali imeuweka ya kuhakikisha kwamba inatoa takwimu halsia na kwa wakati kutoka kwenye vyanzo vyote hivi ili kuweza kuwasaidia watoto wa Kitanzani kujua ukubwa wa tatizo ni nini kuliko ku-base kwenye polisi tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kusua kusua kutokutenga au tukitenga kupeleka fedha kwenye utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilataka kujua ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanatenga bajeti ya kutosha na wanaitekeleza kuhakikisha kwamba kuna kuwa na madawati ya kijinsia ya kutosha kuanzia ngazi ya mitaa, wanawawezesha kuwa na Maafisa Ustawi wa Jamii, Kamati ya MTAKUWWA inapata fedha za kutosha ili kutokomeza hii tatizo kubwa la unyanyasaji wa watoto wa Kitanzania amba wanabakwa, wanalanditiwa, wanauwawa, wanachomwa moto, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, oh Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nimpongeze kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri na ninadhani liko suala linalohusu takwimu za unyanyasaji ataendelea kuzijibbia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninaomba tu nitoe maelezo mafupi kuhusu mkakati huu wa kitaifa wa mapambano dhidi ya unyanyasaji kwa wanawake na watoto kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la kuratibu na kuziunganisha sekta na utekelezaji wake ukifanywa na Wizara yenye dhamana ya Afya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na mkakati wa kwanza ambao ulizinduliwa mwaka 2016 mkakati huo wa MTAKUWA na lengo kubwa ilikuwa ni kukidhi matakwa ya kimataifa lakini matakwa ya Taifa vile vile kuhakikisha kwamba tunaweka sawa masuala haya ya unyanyasaji wa wanawake na Watoto na mkakati huo wa kwanza ndiyo unafikia mwisho, unaelekeea kufikia mwisho mwaka 2021/2022 tutakuwa tumeumaliza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni hivi majuzi tu, wiki mbili zilizopita, nilikuwa kwenye kikao cha wataalam kufanya tathmini ni kwa kiasi gani MTAKUWWA limeweza kufanikiwa. Masuala yaliyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge tumeyaona kwamba ni masuala ambayo yameleta utatanishi kidogo kwa namna moja ama nyingine katika utekelezaji wa MTAKUWWA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namhakikishia kwamba kwenye mkakati wa pili sasa masuala ya bajeti, masuala ya madawati na ya rasilimali watu katika kuhakikisha MTAKUWWA II inafanikiwa na inafikia malengo ambayo yalikusudiwa yanazingatiwa sasa katika mkakati huu uliopita ambao unafanyiwa tathmini, lakini mkakati utakaokuja haya yote yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwape pongezi sana wenzetu wa Jeshi la Polisi. Wameanzisha madawati mengi ya kutosha katika maeneo mbalimbali kwenye vituo vyao vya polisi kwa ajili ya kusaidia kuhakikisha wanawake na watoto wanapata haki zao. Hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa MTAKUWWA kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutakuja muda ukifika tutaomba ushauri, maoni na hata kwa Waheshimiwa Wabunge ili MTAKUWWA II uweze kufanikiwa kwa kadri ya mpango tuliookusudia kuwaokoa wanawake na watoto dhidi ya unyanyasaji katika nchi yetu. Nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, una nyongeza?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, hapana. Naona Mheshimiwa Waziri amekamilisha kila kitu.

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

Na. 93

Vituo vya Afya Kutoza Wajawazito na Watoto

MHE. REGINA N. QWARAY aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia kikamilifu Sera ya Afya ili akinamama wajawazito na watoto wasitozwe gharama katika vituo vya afya?

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa sera na miongozo inayotaka huduma itolewe bure, kumekuwepo na malalamiko ya baadhi ya wananchi walio katika makundi hayo katika maeneo mbalimbali kudaiwa fedha katika vituo vya umma vya kutolea huduma. Ili kuepukana na malalamiko hayo, Serikali inawaagiza Waganga Wakuu wa Mikoa, Waganga Wakuu wa Wilaya, Bodii za Afya na watoa huduma za afya kutekeleza Sera na miongozo inayohusu matibabu bure kwa mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inawakumbusha Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi kuwa ni jukumu lao pia kusimamia miongozo inayotolewa na Serikali. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Regina Qwaray.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Serikali yaliyotolewa hapa, bado kuna tatizo kubwa, hasa kwenye vituo vyetu vya afya, huduma hii imekuwa ngumu sana kwani akinamama wanapokwenda kujifungua wameendelea kutozwa hela na watoto chini ya miaka mitano wanapokwenda pia kupata huduma wameendelea kutozwa fedha. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini ni nini hasa kinakwamisha huduma hii au sera hii isitekelezwe?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; katika vituo vyetu vya afya kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa dawa na vifaa tiba. Je, Serikali ina mkakati gani sasa kuhakikisha kwamba vifaa tiba na dawa zinapatikana katika vituo vyetu vya afya ili watoto wetu na akinamama wanapokwenda kujifungua waweze kupata huduma hiyo? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Dkt. Mollel, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):**
Mheshimiwa Spika, nilijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Regina Ndege kwamba kwa kweli tumeshafanya uchunguzi wa kutosha na kujua kwamba tatizo hilo lipo, ndiyo maana *straight forward* tumetaka kuwaelekeza wanaohusika kufanya kazi yao. Hata kwenye *presentation* ya semina iliyofanywa jana kwa Wabunge wote na Wizara ya Afya tulionesha kwamba *exemption* ile ya akinamama na watoto inachukua asilimia 0.1 mpaka 10.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maeneo ambayo ni 0.1 ni maeneo yale ambayo kwa kweli unakuta akinamama

walitakiwa kupewa hiyo huduma bure na hawapewi; tutakwenda kuboresha kwa nguvu kuhakikisha kwamba huduma inapatikana. Ndiyo maana tumeleta vilivile kwenu ili tushirikiane kwa pamoja ili kuweza kutatua tatizo hilo.

La pili, kwenye eneo la dawa; kwenye eneo hili, Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan alishatoa bilioni 16 na najua Kamati inakwenda siku ya Jumapili, kimejengwa kiwanda kule Njombe ambacho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vidonge vyote vya kutosha nchi nzima kwa siku mbili tu na kimeshafika asilimia 98 kukamilika.

Mheshimiwa Spika, tayari Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya bilioni 185 kwa ajili ya kununua dawa. Tukijumlisha na uelewa ambao jana tulipeana Wabunge wa kusimamia upotevu wa dawa, wanaweza kuona tuna *items* zaidi ya 400 za dawa, lakini tumechunguza tu *items* 20 ndani ya mwaka mmoja kuna upotevu wa bilioni 83. Maana yake tukishirikiana kwa pamoja sisi na viongozi tuliota hapa huko mbele tutaweza kufika hatua nzuri na dawa zikapatikana kwenye maeneo yetu. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, nimekuona.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nami niulize swali dogo la nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi; hii sera ni ya muda mrefu na haitekelezeki. Wabunge mnajua kwenye majimbo yetu, akinamama wajawazito, wazee na watoto chini ya miaka mitano hakuna matibabu bure. Sasa Mheshimiwa Waziri anasema atatoa miongozo, kama hakuna kitu cha kumbana mambo ni yaleyale.

Je, kwa nini kusiwe na sheria kwamba ni lazima akinamama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee wapate matibabu bure ili wazee wasiweke tiba ya kisaikoloja tena, wakienda hospitali wapate matibabu bure? Sera imekuwepo haitekelezeki, leteni sheria kama mna dhamira njema.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Mollel, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na ndio maana umekuwa mkali sana kwenye suala zima la bima ya afya kwa wote. Nataka kukuhanakishia tukienda kutekeleza agizo lako la suala la bima ya afya kwa wote, haya mambo yatakuwa ni historia. Kwa wakati huu miongozo iliyo poto tutaendelea kuifuatilia na kusitiza, lakini Mheshimiwa Ester Bulaya aendelee kushirikiana na sisi ili tuweze kufanya hilo litekelezeke. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea, ni wakati wa Mbunge wa Kilolo sasa, uliza swali lako Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 94

**Hitaji la Umeme Kata za Nyanzwa, Udekwa na
Ukwega – Kilolo**

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme katika Kata za Nyanzwa, Udekwa na Ukwega Wilayani Kilolo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilolo ina kata 21, kati yake kata tatu tu havijapata umeme na vijiji 94, kati yake vijiji 23 tu havijapata umeme. Vijiji vyote 23 ambavyo havina

umeme vikiwemo Vijiji vya Kata za Nyanzwa, Udekwa na Ukwega ambavyo ni Nyanzwa, Mgowelo, Igunda, Udekwa, Wotalisoli, Ifuwa, Ukwega, Ipalamwa, Makungu na Mkalanga vinapatiwa umeme kuitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambao utekelezaji wake uliana mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo, nimekuona.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nakiri ni kweli nimeona kazi hiyo inaendelea katika kata hizo zilizotajwa. Pamoja na hayo nina maswali yangu mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza; katika utekelezaji wa miradi hii maeneo mengi ya huduma za jamii, hasa shule za msingi, shule za sekondari, makanisa na misikiti, hasa maeneo ambayo yako mbali kidogo na katikati ya miji, haziwekewi kipaumbele sana kupata umeme. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kutenga bajeti maalum kwa ajili ya huduma za jamii, hasa sehemu ambazo watoto wetu wanasoma kwa sababu ni muhimu sana kuwa na umeme?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; katika miji mbalimbali midogo kwa mfano Mji wa Ilula uliopo Kata ya Nyalumbu, lakini pia Mji Mdogo wa Boma la Ng'ombe pamoja na Mji Mdogo wa Kidabaga, kumekuwa na kero kubwa ya kukatika umeme mara kwa mara. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza kero hii? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye utekelezaji wa Mradi wa *REA III*, Mzunguko wa Pili,

tuliwaelekeza wakandarasi wanaopeleka umeme katika maeneo yetu pamoja na wale wanaoshirikiana nao, wenzetu wa *TANESCO*, kuhakikisha kwamba maeneo ya taasisi na miundombinu mingine kama elimu, afya na taasisi za dini yanakuwa ni maeneo ya kipaumbele. Kama alivyosema Mheshimiwa Nyamoga, ni kweli maeneo yale ambayo tayari umeme umeanza kwenda kwenye maeneo ya makao makuu ya vijiji tayari tunapeleka.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Nyamoga pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba kadri tunavyozidi kupeleka umeme kwenye maeneo ya pembeni kwa maana ya vitongoji, tutazidi pia kufika katika taasisi hizo na ni maelekezo ya Serikali kwamba umeme ufile katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Jambo lingine la kufurahisha zaidi ni kwamba, sisi Wizara ya Nishati pia tumepewaa kipande kidogo cha bajeti katika ile 1,300,000,000 za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan zinazopeleka maeneo ya UVIKO tunaopambana nao na sisi katika miundombinu hiyo mipya ambayo inajengwa tumepatiwa pesa kiasi fulani ambapo tutaweza kuongeza kasi ya kupeleka umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili, ni kweli kwamba kumekuwa kuna makatizo ya umeme kwenye maeneo mbalimbali, lakini ni jambo ambalo liliopangwa kwa ajili ya kufanya marekebisho ya miundombinu. *TANESCO* katika mwaka huu wa fedha inazo bilioni karibu zaidi ya 200 kwa ajili ya marekebisho ya miundombinu ya umeme katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge waendelee kutuvumilia kidogo tukiwa katika hatua hizi na harakati za kuhakikisha tunaboresha miundombinu yetu. Na kwa Iringa tuna takribani bilioni moja na milioni 500 kwa ajili ya marekebisho ya miundombinu. Tutaendelea kuwashimiza wenzetu watoe taarifa sahihi na kwa wakati

sahihi ili Waheshimiwa umeme unapokatika, basi wananchi waweze kufahamu nini kinaendelea. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, nimekuona.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba niulize swal dogo tu la nyongeza. Kuna Mkandarasi anaitwa Giza mlituletea kwenye majimbo yetu, na milimpa siku za kuja kwa Wabunge, mpaka leo tunamtafuta; nini kauli ya Serikali? Ahsante sana.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza ukatutafutia huyo mkandarasi wenu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ni kweli nimepata *concerns* za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Mkandarasi huyu Giza na kama alivyowahi kusema Mheshimiwa Mbunge mmojawapo kwamba jina la mkandarasi halivutii, lakini ni mmoja wa wakandarasi ambao walipata kazi katika Mradi wa *REA II, round two* katika Mikoa ya Manyara na Mara.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wamekuwa wakinuuliza mara kwa mara. Nitoe taarifa kwamba, tumemtafuta na tumempa maelekezo mahususi, nikitoka hapa nitawaeleza Waheshimiwa Wabunge ni namna gani tumechukua hatua ili aweze kufanya kazi yake na kuimaliza, ili inapofika hiyo Desemba 2022 ambayo tumekubaliana naye, tusiwe nje ya muda huo.

SPIKA: Kama mkandarasi Giza amepatikana, hayuko gizani tena, sasa muunganishe na Wabunge.

Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Magharibi, nilikuona.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ili niulize swal dogo tu la nyongeza. Ni lini sasa mkandarasi ambaye majuzi tu

Mheshimiwa Naibu Waziri alituambia hapa katika Bunge lako Tukufu kwamba anaanza kazi katika Halmashauri za Wilaya za Manyoni na Itigi ataanza kazi?

SPIKA: Majibu mafupi ya hilo swali; lini anaanza kazi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaelekeza wakandarasi wa *lot* hizo nne ambazo zilikuwa zimebakia, waripoti katika vituo vyao vya kazi wiki hii inayokwisha leo na ilikuwa ni kwenda kuangalia maeneo ya kupata *go down* za kutunza vifaa vyao na kuwasiliana na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge hajawasiliana na mkandarasi wake, naomba nitakapotoka hapa mimi mwenyewe nimuunganishe naye. Wiki inayokuja tunatarajia waanze kwenda kwenye maeneo hayo kwa ajili ya *survey* na kuanza kazi ambazo wameshasaini mikataba tayari. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mtaturu, Mbunge wa Ikungi, nilikuona.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Yapata miezi sita sasa tuliambiwa kwamba mkandarasi ataanza kazi na sisi tulipewa jina, anaitwa *Central*. Mheshimiwa Naibu Waziri nimeongea naye mara mbili akiniambia yuko njiani anakuja. Nafikiri ametoka mbali sana, mpaka sasa hajafika. Naomba sasa Waziri atuambie, ni lini atafika katika Jimbo la Singida Mashariki?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali hasa msingi wake ni kwamba hawa wakandarasi wenu ambao mmekuwa mkiliambia Bunge hawajafika. Yaani hiyo ndiyo *message*. Naomba tu uipokee muifanyie kazi hiyo *message*; hawajafika *site*, huo ndiyo ujumbe ambao naomba muupokee. (*Makofii*)

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara.

Na. 95

Tatizo la Maji Safi Ngara Mjini

MHE. NDAISABA G. RUHORO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la maji safi katika maeneo ya Ngara Mjini pamoja na maeneo ya jirani ya Murukulazo, Nyamiaga, Muruguanza na Buhororo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji Safi Ngara?

SPIKA: Tuko kwako Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Ngara ni wastani wa asimilia 63. Uzalishaji wa maji ni mita za ujazo 1,500 kwa siku ambapo mahitaji ni mita za ujazo 2,500.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Ngara, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali itachimba kisima kirefu chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 80,000 kwa saa, kukarabati mtandao wa bomba umbali wa kilomita 1.73 na kuongeza mtandao wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 1.5. Kazi hizo zitaanza kutekelezwa mwezi Desemba, 2021 na kukamilika mwezi Aprili, 2022. Kukamilika kwa kazi hizo kutaboresha huduma ya maji katika Mji wa Ngara kufikia asilimia 78.9.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu ni kujenga mradi mkubwa wa maji utakaotumia chanzo cha

Mto Ruvuvu. Mradi huo utanufaisha Mji wa Ngara na maeneo/Vijiji vya jirani vya Nterungwe, Nyakiziba, Kumutana, Mayenzi, Mukirehe, Murukulazo, Nyamiaga, Muruguanza na Buhororo. Kazi ya usanifu imepangwa kukamilika katika robo ya pili ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi anatarajiwa kupatikana kabla ya mwezi Julai, 2022.

SPIKA: Mheshimiwa Ndaisaba, nimekuona.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya maji umekuwa ukitumia wakandarasi; na kwa kuwa wakandarasi hawa wanachukua muda mrefu sana kukamilisha miradi hii ya maji; na kwa kuwa yuko mkandarasi alipewa mradi aumalize ndani ya mwaka mmoja na sasa ni mwaka wa sita unakwenda wa saba hajakamilisha mradi huo; na kwa kuwa mimi nia yangu ni kuhakikisha miradi yote ya maji niliyoshiriki kuitisha fedha Bungeni hapa inakamilika ndani ya kipindi cha miaka mitano. Je, Serikali inaweza kuturuhusu kutumia *force account* kutekeleza Mradi huu wa Maji wa Ngara Mjini na miradi mingine ili miradi hii ikamilike kwa wakati, tena ndani ya kipindi cha miaka mitano? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpungeza sana Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, amekuwa ni mfuatiliaji na ye ye mwenyewe amekuwa akienda mbele zaidi katika shughuli hizi za miradi ya maji. Hata nilipomtembelea pale jimboni, alionesha jitihada kubwa sana ya kuona kwamba miradi inakamilika.

Mheshimiwa Spika, kutumia *force account* ni moja ya namna ambavyo tunatekeleza miradi yetu sisi Wizara ya Maji.

Hivyo, katika miradi hii ambayo imechukua muda mrefu, tayari miradi zaidi ya 100 tumeweza kuruhusu *force account* na imekamilika. Hivyo na huu nao tunaupokea, tutahakikisha wenzetu waliopo pale Ngara na wao wanafanya jitihada ya kuona mradi unakamilika. Ahsante.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Innocent Bilakwate, uliza swali lako.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nipongeze Wizara ya Maji kwa juhudini zinazoendelea za kuwapatia wananchi wa Jimbo la Kyerwa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kyerwa tunao Mradi wa Vijiji 57, lakini mradi huu tumekubaliana utajengwa kwa awamu. Hata hivyo, zipo Kata kama Businde, Songa Mbele, Kikukuru, Kitochenkula; kata hizi haziko kwenye awamu hii ya kwanza. Je, Serikali iko tayari angalau hata kuchimba visima ili hawa wananchi ambao wanapata wakati mgumu waweze kupatiwa maji safi na salama wakati wanasubiria mradi mkubwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna mradi mzuri sana pale kwenye Jimbo la Kyerwa na Mheshimiwa Innocent amekuwa bega kwa bega na Wizara. Tumekuwa tukishirikiana naye sana Mheshimiwa Mbunge. Kwa visima kuchimbwa kwa dharura wakati miradi mikubwa ikiendelea na utekelezaji, hii ni moja ya jitihada za Wizara na tumetenga zaidi ya visima 500 kuona kwamba tunavichimba katika maeneo ambayo miradi yake inachukua muda mrefu. Hivyo, kwa kata hizi

ambazo ziko pembezoni kwenye Jimbo la Kyerwa nalo tutalifikiria kuona visima vinachimbwa.

SPIKA: Mheshimiwa Condester Sichalwe, nimekuona.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Jimbo la Momba lina vijiji 72 na vitongoji 302. Katika vijiji hivyo, vijiji ambavyo vinapata majisafi na salama ambayo yanafaa kwa matumizi ya binadamu haviwezi kuzidi 20; isipokuwa tunatumia mbadala wa maji ambayo yametuuma kwenye madimbwi na kwenye mito midogo midogo ambapo tunakunywa pamoja na ng'ombe, punda, mbuzi na wanyama wote:-

Je, ni lini Serikali itaona katika vijiji vilivyobaki, watusaidie kutuchimbia visima vyta dharura wakati tunaendelea kusubiri miradi mikubwa ya maji ili tuendelee kupata maji safi na salama kama ambavyo binadamu wengine wanapata maji safi na salama? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester, Mbunge wa Jimbo la Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Jimbo la Momba bado lina changamoto ya maji na ni moja ya maeneo ambayo yapo kimkakati katika Wizara na tumetupia jicho la kipekee kabisa pale. Visima ni moja ya miradi ambayo tunakuja kutekeleza ndani ya Jimbo la Momba. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, tutakuja kutekeleza wajibu wetu, kwa sababu wananchi wale pia wapo Tanzania. Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan, amesema wanawake wote lazima tuwatue ndoo kichwani. Mantahofu, tunakuja kufanya kazi Momba. (*Makof*)

SPIKA: Tunahamia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi, tafadhalii.

Na. 96

Ujenzi wa Barabara ya Bihawana – Bahi - Manyoni

MHE. KENNETH E. NOLLO aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Bihawana – Chali hadi Sanza Manyoni kwa kiwango cha lami kwa kuwa barabara hii muhimu huwa haipitiki wakati wa masika?

(b) Je Serikali ina mpango gani wa kuinua tuta la barabara katika eneo la Chali ili liweze kupitika wakati wote?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri Mhandisi Msongwe, tafadhalli.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bihawana – Chali hadi Sanza Manyoni ni barabara ya Mkoa inayojulikana kwa jina la Bihawana - Chidilo – Chipanga – Chali Igongo ambayo ina urefu wa kilomita 69, ambayo inaunganisha Wilaya za Bahi na Manyoni kupitia Sanza. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kufanya upembusi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha za kufanya upembusi yakinifu na usanifu wa kina ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha wa

2021/2022 shillingi milioni 759.252 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu (b) kuhusu kuinua tuta eneo la Chali, Serikali imefanya kazi zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Serikali imejenga kalavati kubwa na kuinua tuta lenye urefu wa mita 500. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Serikali imejenga makalavati makubwa mawili na kuinua tuta lenye urefu wa mita 100. Vilevile, katika mwaka wa fedha huu wa 2021/2022, Serikali imepanga kunyanya tuta lenye urefu wa mita 500 ambapo mkataba wa kazi hii upo katika hatua za kusainiwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Nollo, swali la nyongeza.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kutokana na umuhimu wa barabara hii Wabunge wengi waliopita upande wa Bahi na upande wa Manyoni, wamekuwa wanaulizia kuhusu umuhimu wa barabara hii na majibu ya Serikali yamekuwa ndiyo hayo, kwamba, tunatafuta fedha kwa ajili ya usanifu yakinifu na ile nyingine alioisema.

Mheshimiwa Spika, sasa, tena niulize hapo: Je, ni lini fedha ya upembuzi yakinifu itapatikana? Maana yake ndiyo hayo miaka yote. Sasa ile ya upembuzi yakinifu na ile nyingine, ni lini fedha itapatikana? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwenye majibu ya sehemu (b) nilikuwa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri afanye ziara ili aweze kupata uhakika kabisa na alichokijibu hapa. Mimi mwezi wa Nne nilikesha pale, barabara ilijifunga na kinachojibwa hapa sicho kilichofanyika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Bunge hili hebu akafanye ziara aweze kuona na mwenyewe awe na picha halisi ya eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Ungemsubirisha kidogo mvua inyeshe halafu ndiyo uende naye. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri Mhandisi Msongwe, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini? Serikali mwaka huu wa fedha imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza kazi hii. Suala la kutembelea, hilo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, niko tayari kutembelea hilo eneo kwa sababu ni eneo hili hili tu. Nitakapokuwa nakwenda Kaskazini, basi nitapita barabara hiyo na nitamjulisha ili tuweze kukagua pamoja naye hiyo barabara. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Amar, Mbunge wa Nyang'hwale.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa leo ni mwaka wangu wa 12 nikiwa Bungeni, Rais wa Awamu ya Nne alituahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kahama, Nyang'hwale mpaka Busisi na Rais wa Awamu ya Tano naye pia aliahidi hivyo, na leo tuko Awamu ya Sita.

Je, Serikali inatuahidi nini ama inatoa kauli gani kuweka fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya hiyo barabara?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara zote ambazo zimeahidiwa na viongozi wa Kitaifa zinakuwa zimeratibwa na zinahafanyiwa kazi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Kahama kupita Nyang'hwale hadi Busisi ni kati ya barabara ambazo zipo kwenye Mpango na zitaanza kutekelezwa kadri fedha itakavyopatikana. Labda tuangalie kwa bajeti itakayofuata kama fedha itaruhusu na bajeti itaruhusu, basi tutaiweka kwenye Mpango huo ili iweze kufanyiwa upembuzi na usanifu wa kina. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Chaya, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Barabara ya Bihawana, Chali, Sanza, Manyoni ambayo imeulizwa na Mheshimiwa Nollo ili iweze kukamilika inahitaji ukamilishaji wa ujenzi wa Daraja la Sanza; na kwa taarifa yako upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishakamilika na fidia ilishatolewa kwa wananchi wa Kijiji cha Sanza:-

Je, nini *commitment* ya Serikali ya lini ujenzi wa daraja la Sanza utaanza? Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante. Majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mbunge wa Manyoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli daraja analosema limeshafanyiwa usanifu na litagharimu pamoja na barabara zake za kuingilia shilingi bilioni 23 na barabara zitakazojengwa ni kilomita kama 14.5. Tunavyoongea, tayari tumetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza hiyo kazi. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Tuhamie Kilimo sasa. Mheshimiwa Mbunge wa Kwela Mheshimiwa Deus Sangu, uliza swali lako.

Na. 97

Kukamillisha Miradi ya Umwagiliaji – Kwela

MHE. DEUS C. SANGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Miradi ya Umwagiliaji ya Illemba, Ng'ongo, Maleza, Mititi, Itela, Illemba na Nkwilo katika Jimbo la Kwela?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mpango wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Wilayani (*DIDF*), kwa mwaka 2008/2009 na mwaka 2009/2010 ilitenga jumla ya shilingi milioni 650,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza skimu ya umwagiliaji ya Ng'ongo, yenye ukubwa wa hekta 650 ambazo ujenzi ulianza kutekelezwa mwaka 2012 na kukamilika mwaka 2013. Fedha hizi zilitumika kujenga banio na mfereji mkuu wenye urefu wa mita 1,725 pamoja na miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupitia (*ASDP II*) imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwenye skimu ya umwagiliaji ya Illemba yenye ukubwa wa hekta 800. Aidha, kazi ya kupima mashamba imekamilika na usanifu wa kina upo hatua za mwisho katika skimu ya umwagiliaji ya Illemba.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanza kufanya tathmini ya kina katika miradi yote ya umwagiliaji katika Mikoa ya Rukwa na Katavi. Tathmini hiyo ni pamoja kuangalia kwa kina upungufu kwenye skimu hizo na kutambua maeneo mapya na pia kufanya usanifu wa kina na kutathmini gharama za ujenzi wa miundombinu hiyo ili kuanza kutenga fedha katika bajeti zijazo.

SPIKA: Mheshimiwa Sangu, nimekuona.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu hayo yenye matumaini makubwa nataka kujuua: Je, ni lini mtaanza ujenzi wa Skimu ya Illemba ambayo usanifu wa kina uko hatua za mwisho, ikiwa ni pamoja na kumalizia skimu ya Ng'ongo na skimu ya Sakalilo ambazo zimetelekezwa kwa muda mrefu sana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nataka kujuua pamoja na kutambua skimu ya Mititi, Illemba na Itela, ni lini mtaanza upembuzi yakinifu kwenye skimu hizo muhimu kwa wananchi wa Kata hizo nilizozitaja?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kuhusu hizo skimu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sangu, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba skimu hizi kwa muda mrefu zimekuwa *idle* na hazijafanya kazi yake kwa kiwango ambacho kinatarajiwu. Matatizo mengi ya mifumo yetu ya umwagiliaji imekuwa kwamba skimu nyingi zinajengwa na zinaishia njiani ama zinajengwa mifereji bila kuwa na vyanzo vya uhakika vya maji. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo nilitaka nimwahidi kwamba skimu ambazo tumeshazifanyia usanifu, tutaanza kuzitengea fedha kuanzia bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nimpe *commitment*; nilimwahidi tulipokuwa wote Rukwa na ninamwahidi tena mbele ya Bunge lako kwamba skimu hii ambayo usanifu wake upo kwenye hatua za mwisho, ni moja kati ya skimu za Mkoa wa Rukwa ambazo tumeshaziweka katika bajeti ya mwaka kesho. Kwa sababu, usanifu tuliofanya ni usanifu kamili kuanzia chanzo cha maji na mifereji mikuu na mifereji ya *primary* na *secondary canals*.

Mheshimiwa Spika, la kuhusu kwa ujumla, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi kama Wizara na wiki hii iliyopita Waziri wa Kilimo alituagiza tukae na Tume ya Umwagiliaji. Tumeanza utaratibu mpya kabisa kwenye mifumo ya umwagiliaji kwamba hatujengi skimu nusu nusu, ni heri tujenge skimu moja katika Mkoa kwa ukamilifu, badala ya kupeleka hapa shilingi milioni 50 pale shilingi 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watusubiri tunavyoleta katika bajeti yetu itakayokuja, tutahakikisha Ofisi za Mikoa za Umwagiliaji zinapewa uwezo. Vile vile tutakwenda kufungua Ofisi za Umwagiliaji katika kila Wilaya ili ziweze kusimamia skimu na kuzitambua skimu zote ambazo zipo katika Wilaya zetu. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Eric Shigongo, nimekuona.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa yanayomkuta Mheshimiwa Sangu huko Kwela yanafanana kabisa na yanayotokea huko Jimboni Buchosa; na kwa kuwa kilimo sasa kimeshathibitika kwamba ni uti wa mgongo na unategemewa na Taifa letu:-

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutembelea skimu ya Uchiri iliyopo Buchosa ambayo imetelekezwa kwa muda mrefu, akiwa katika utaratibu wa kuifufua iweze kuwasaidia wananchi wa Buchosa na Taifa kwa ujumla? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niko tayari kwenda kutembelea Jimbo la Buchosa na niko tayari kwenda kutembelea Jimbo la Sengerema kuangalia mabwawa, ambayo fedha zake zilitolewa na hayajafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, tutashirikiana Waheshimiwa Wabunge, tutakwenda pamoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi, nimekuona.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika skimu ya Mng'aro ambayo Mheshimiwa Waziri mara kadhaa hapa alikuwa anaitolea maelezo; na nimeiuliza lakini bado mpaka sasa fedha zile ambazo mmezitenga shillingi milioni 30 hazijafika kuboresha banio na sasa tunaelekea kuanza kwa msimu wa kilimo:-

Je, ni nini *commitment* ya Serikali katika jambo hill?

SPIKA: Majibu ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi. Kwanza nimpongeze sana ye ye binafsi pamoja na Diwani wake Ndugu Jambia Juma Shehoza kwa kuifuatilia Skimu ya Mnga'ro.

Nataka tu nimwambie kwamba tumeshatangaza *tender* tarehe 18 Novemba, 2021 *tender* hiyo inafunguliwa ili kupatikana Mkandarasi wa kuweza kwenda kuifanya kazi na kurekebisha tatizo la skimu hiyo. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, nimekuona.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru leo kwa kuniona pamoja na ufupi wangu. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, leo umesimama. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ninayoiona katika utengenezaji wa hizi skimu ni ukosefu wa wataalam. Kwa mfano, nimeshtuka sana kujua kwamba Skimu ya Sakalilo mpaka leo eti haijakkamilika. Yaani toka kipindi hicho mimi nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, wataalam walikuwa wanatoka Mbeya miaka ya 2013 mpaka leo haijakkamilika. Kuna tatizo kubwa sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba nifahamishwe, Wizara imejipanga vipi kupata wataalam wa kutosha ili kusaidia hizo skimu? (*Makofi*)

SPIKA: Mmejpangaje Mheshimiwa Naibu Waziri? Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza tuliyofanya kama Wizara, kama alivyosema kwamba wataalam walikuwa wanatoka Mbeya. Sasa hivi tumevunja ofisi za kanda na sasa kila Mkoa una Ofisi ya Tume ya Umwagiliaji na tumepeleka *manpower*, kwa maana ya *ma-engineer* na kila Mkoa sasa una *engineer* wa umwagiliaji. Hivi karibuni tumewaruhusu *ma-engineer* wetu wa Tume ya Umwagiliaji, kuajiri *intense* ambao ni *graduates* kutoka *University* ambao ni *ma-engineer* wa *irrigation* waweze kwenda *ku-beef up* Ofisi za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ambayo tunajipanga nayo ni kuhakikisha katika kila Wilaya tunakuwa na *engineer* wa umwagiliaji tukishirikiana na waliopo katika TAMISEMI ili tuweze kuhakikisha kwamba shughuli za umwagiliaji zinasimamiwa. Kwa mwaka ujao wa fedha tutakuwa na ofisi katika kila Halmashauri inayosimamia suala la umwagiliaji ili

kuwe kuna *efficiency* katika kufuatilia miradi ya umwagiliaji na *ku-plan* ili siku ya mwisho tusifanye kazi hizi nusu nusu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na miradi mingi ya umwagiliaji ambayo iko chini ya kiwango ambacho kinachotarajiwa na hili ni suala la *planning* na *resource*. Nasi kama Wizara tumepeleka mapendekezo yetu Hazina. Tunaamini mwaka ujao wa fedha na Waziri wa Fedha alisema ndani ya Bunge lako wakati anahitimisha kwamba umwagiliaji utakuwa ni sehemu ya kipaumbel. Tunaamini itakuwa hivyo na Bunge lako litatupatia rasilimali.

Mheshimiwa Spika, hatuna tatizo la wataalamu, tuna tatizo la rasilimali fedha ambayo tumeshapeleka kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha ili tuweze kutatua hili tatizo. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali iliahidi kufanya mapitio ya usanifu wa ujenzi wa bwawa la umwagiliaji kwenye eneo la Mto Mkomazi kule Korogwe, lakini mpaka leo ahadi hiyo bado haijatekelezwa:-

Napenda kujua, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa bwawa hilo, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa watu wa Korogwe?

SPIKA: Majibu ya swali hilo pia.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava. Tulifanya ziara akiwepo Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Jimbo lake na tuliahidi kupeleka wataalamu.

Nataka tu nimwambie kwamba Wizara ya Kilimo imepatiwa fedha kwa ajili ya Tume ya Umwagiliaji, *OC* tumeshapokea. Sasa moja ya eneo ambalo wataalam wetu na wasanifu wanakwenda kulifanya kazi ni eneo hilo. Kwa

hiyo, nataka nimhakikishie tu kwamba kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha usanifu wa bwawa hilo utakuwa umekamilika na tutaliingiza katika *plan*. (*Makof*)

SPIKA: Sasa nimekuona Mheshimiwa, uliza swali lako. (*Kicheko*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Changamoto ya skimu zilizopo Jimbo la Kwela kama ulivyomsikia Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya akiwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa; Serikali iliwekeza fedha nyangi kwenye miradi miwili; skimu ya Lwafi pamoja na Katongoro lakini yote haifanyi kazi:-

Mheshimiwa Spika, napenda kupata kauli ya Serikali; Serikali iliwekeza zile fedha zipotee au iliwekeza ili ziwasaidie Watanzania wa Wilaya ya Nkasi? (*Makof*)

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Aida Khenani Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali hajjawekeza fedha zile ili zipotee na mapungufu yeye mwenyewe anafahamu, nilikuwa Jimboni kwake na tumeongea kwa kina kuhusu hizi *scheme* zilizoko katika Jimbo lake, sasa hivi kama Wizara tunafanya hatua za mwisho kupeleka fedha tuliyokuahidi ya Shilingi Milioni 100 ili fedha hizo ziweze kwenda.

Nataka tu nimuahidi kwamba mapungufu yaliyopo katika *scheme* zilizoko Mkao wa Rukwa na sehemu nyangi ya nchi ni kwamba nyangi zimejengwa *half way*, kwa hiyo sasa hivi tunachokifanya ni kuzifanyia tathmini ili tuweze kuzirekebisha ziwe zinachanzo cha maji cha uhakika na mifereji, *scheme* nyangi zimejengwa mifereji badala ya kuwa na *water reserve*, kwa hiyo nataka nimuombe yeye pamoja na Waheshimiwa Wabunge, mtupe nafasi ili tuweze *ku-rectify* haya matatizo yaliyopo. (*Makof*)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo na ndiyo linalotufungia shughuli za Mkutano wa Tano, sasa ni Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Charles Mwijage.

Na. 98

Serikali Kuhamasisha Kilimo cha Zao la Chikichi

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE aliuliza: -

Nchi yetu imekuwa na mipango mkakati wa kuzalisha mafuta ya kula kiasi cha kutosheleza soko la ndani.

(a) Je, ni kwa nini Serikali isiboreshe mpango ya kuzalisha mafuta ya mawese kimkakati kwa kuhamasisha kilimo cha zao hilo katika Mikoa ya Kagera, Tanga, Pwani, Katavi na Mbeya;

(b) Je, ni kwa nini Serikali isitumie mfumo wa kilimo kikubwa cha pamoja (*block farming*) ambapo Serikali hubeba gharama za awali na hatimaye sehemu ya gharama hukatwa kwenye mauzo ya Mkulima.

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tupo kwako Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ya Kagera, Tanga, Pwani, Katavi na Mbeya na Halmashauri za Mikoa hiyo inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa zao la michikichi katika maeneo yanayofaa kuzalisha zao hilo.

Uhamasishaji huo ni pamoja na kuzitaka Halmashauri hizo kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche bora ya michikichi aina ya Tenera, kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalam kuhusu kilimo bora cha michikichi na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kat i vya kuchakata mafuta ya mawese jirani na maeneo ya uzalishaji ili kusafirisha mikungu ya michikichi kwenda viwandani.

Mheshimiwa Spika, kutohana na uhamasishaji huo baadhi ya Halmashauri za Wilaya zimeanzisha vitalu vya kuzalisha miche bora ambapo Ngara (Kagera) immeanzisha kitalu cha miche 100,000; Mkuranga (Pwani) miche 20,000; Tanganyika (Katavi) miche 70,000 na Kyela (Mbeya) miche 26,600.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri zenyenye maeneo makubwa yanayofaa kwa kilimo cha michikichi inaendelea kuhamasisha kilimo cha mashamba ya pamoja (*Block farming*) ili kuzalisha kwa tija na kurahisisha huduma kwa wakulima. Baadhi ya Halmashauri hizo ni Uvinza (Kigoma) ekari 5,000 na Uyui (Tabora) ekari 12,000. Uhamasishaji unaendelea kwa mikoa mingine yenye sifa hizo.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Charles Mwijage uliza swali la nyongeza.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuanzisha *block farming* kwenye maeneo aliyooyataja kama kwetu Kigoma, maeneo yanayotengwa yanauzwa kwa watu kwamba hekari Tano njoo utoe pesa, lakini mojawapo ya lengo la *block farming* ni kuwagawia wale wananchi ambaon dio walikuwa wazalishaji wakubwa kwamba Serikali muwabebe halafu mkiwabeba kwa gharama za Serikali ile pesa mliowekeza wananchi watairudisha unapouza.

Kwa nini Serikali sasa msjiandae mkafungua maeneo makubwa mukawatoa Watanzania kwenye nusu heka kwa kaya mkawapeleka heka tano na mkavumilia tunapouza kwa sababu haya mazao ya kimkakati, tutakapouza tukaweza kurudisha hizo pesa kwenye Mfuko wa Serikali? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwijage kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, dhana ya *block farming* kama alivyoieleza ina njia mbili, aidha Halmashauri ikitenga eneo watu wenye uwezo waweze kununua kuwekeza na kumilikishwa eneo hilo, lakini njia nyingine ni eneo ambalo ardhi inakuwa ni mali ya Halmashauri halafu Wawekezaji wanakuja kuwekeza kwa kupewa *long term leasing* ambayo wao wanawekeza.

Kwa hiyo, nilitaka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba kama Wizara tuko tayari kukutana na Halmashauri yoyote ambayo itakuwa tayari kujadiliana na sisi tutengeneze *module* ambayo ita attract watu wengi kuweza kuwekeza katika eneo hilo na hilo ni wazo ambalo tunalipokea na tuko tayari kuweza kujadiliana kuweza kufanikisha jambo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa kunti uwe muuliza swali wa mwisho jioni ya leo.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa kupunguza uhaba wa mafuta nchini pamoja na zao la mchikichi lakini Serikali ilitangaza zao la alizeti kuwa ni zao pia litakaloingia kwa ajili ya kwenda kupunguza uhaba wa mafuta ya kula nchini. Katika mkakati huo wa Serikali Waziri Mkuu alitangaza

Mikoa mitatu Mikoa wa Dodoma, Singida pamoja na Simiyu kuwa ndiyo Mikoa itakuwa kinara cha uzalishaji wa zao la alizeti.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo kwenye zao hili ni upatikanaji wa mbegu bora pamoja na gharama nafuu, sasa nilitaka kujua Serikali ama Wizara wamejipangaje kwenye suala zima la upatikanji wa mbegu bora ambayo pia itakuwa ni bei nafuu itakayoweza kukidhi wakulima wetu kuweza kupata mbegu hiyo?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata majibu ya Serikali kuhusiana na zao hili la alizeti. (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu kuhusu alizeti.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali tulitangaza zao la halizeti kuwa zao la kimkakati na sisi kama Wizara, ni vizuri Bunge lako Tukufu likafahamu kwamba tumetangaza Mikoa mitatu kuwa ni Mikoa kinara ikiwepo Dodoma, Singida na Simiyu. Hatua tulizochukua kwenye suala la mbegu, Wizara tumeshaandaa jumla ya tani 1,600 za *standard seed* ya *record* ambayo tunaiiza kwa shilingi 3.500. Tulichokitaka kutoka kwenye Halmashauri husika ni Halmashauri ilete mahitaji ije tuipatie mbegu, watasaini *petition* ya makubaliano na Wizara ya Kilimo kuonyesha kwamba hiyo *subsidies rate* ya shilingi 3,500 fedha yake italipwa namna gani.

Mheshimiwa Spika, tumetoa aina tatu ya namna ya kulipa, *cash 50 percent* ama kulipa mwisho baada ya mkulima kuvuna, tunawaomba Wakurugenzi wa Halmashauri za Dodoma, Singida na Simiyu tumeshasema tumeongea na Wakuu wa Mikoa na leo tumewaambia Wakuu wa Mikoa tulipokuwa nao kwenye kikao walete. Mheshimiwa Mbunge

na wewe karibu umlete Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chemba aje tuweze kukubaliana namna ya kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu *long term* sisi kama nchi tunahitaji *high breed seed* zaidi ya tani Elfu Tano ili tuweze kuipeleka kwa wakulima. Kwa hiyo, hatua tunayoichukua kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha ni kwamba tutaingia mikataba na wazalishaji binafsi, watu binafsi siyo lazima tuzalishé mbegu Serikali, tutasaini nao makubaliano na wapo watu ambao wameshajitokeza mfano ni mtu anaitwa Ndugu Sumri ambae ana jumla ya hekta 8,000 kule Rukwa tunaingia nae makubaliano tunampa *parent seed* ye ye anatuzalishia sisi serikali, halafu zile mbegu ndiyo tutazi-*subsidies*ili wakulima waweze kuzipata, ili tuondoke kwenye *vicious cycle* ya mbegu ni lazima turuhusu sekta binafsi ishirikiane na Serikali na huo ndio mwelekeo wa Wizara, tunaamini baada ya mwaka mmoja ama miwilli tatizo la mbegu za alizeti katika nchi litakuwa historia.

SPIKA: Waheshimiwa wa sababu ya muda..

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Baada tu ya matangazo nitapokea huo Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao Bungeni mchana huu ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya mkesha mkubwa wa maombi ya Kitaifa wa Kanisa la Tanzania *Fellowship of Churches (TFC)* Askofu Dkt. Godfrey Emmanuel Malassy kutoka Jijini Dar es Salaam, Askofu Malassy, ahsante sana Baba Askofu tunakukaribisha sana. Askofu Malassy pamoja na wenzake wameandaa mkesha mkubwa katika Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma ambao utafanyika tarehe 31 Disemba na mkesha huu utahudhuriwa na Watanzania wote wa dini mbalimbali na Viongozi wa Kitaifa watakuwepo, kwa hiyo, tunaalikwa Waheshimiwa Wabunge tutakaokuwepo Dodoma siku ya mkesha wa tarehe 31 kwenda tarehe Mosi kushirikiana na Baba Askofu na timu yake ya Tanzania *Fellowship of Churches (TFC)* katika uwanja wa

Jamhuri Dodoma kwa ajili ya mkesha huo. Ahsanteni sana na mbarikiwe na Bwana kwa maandalizi hayo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Baba Askofu ameambatana na Mchungaji Daudi Kuselya ahsante. Mchungaji Rose Aman, ahsante. Mchungaji Daniel Shangali, ahsante na Mchungaji Agness Ngogomba, ahsanteni sana na karibuni sana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu ambae ni Dada yake kutoka Songea Mkoani Ruvuma Ndugu Genofeve Mpopo yuko wapi, ndio upo pale ok, ahsante sana karibu sana karibu Dada, sasa na ye ye hajatufafanulia ni Dada mkubwa au Dada Mdogo lakini wote ni Wangoni hawa hawa unajua, ahsante sana Dada Genofeve.

Wageni 40 wa Mheshimiwa Khamis Chilo Naibu Waziri wa Mambo Ndani ya Nchi kutoka Jimboni Uzini ambaao ni vijana wa timu ya mpira wa miguu ya *Chilo Combine* iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja wakiongozwa na Katibu wa Jimbo Ndugu Vuai Simai, *Chilo Combine* karibuni sana bahati mbaya mmefika siku ya mwisho karibu tunaondoka tungewapa kazi na kucheza na timu ya Bunge nafikiri sijui mngerudi na kapu ya magoni kule Zanzibar, lakini karibuni sana rafiki zetu kutoka Visiwani na Mheshimiwa Naibu Waziri anafanya kazi nzuri hapa Bungeni. (*Makofi*)

Wageni wa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambaao ni Wajumbe Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kilimo Biashara na Utalii kutoka Zanzibar mpo? Ok karibuni sana. Sasa naomba mkae niwatambue mmoja mmoja, kwanza Mwenyekiti Mheshimiwa Yussuf Iddi karibu sana, Makamu Mwenyekiti Ndugu Azza Joseph ahsante, Mjumbe ambae ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Mheshimiwa Omar Shaaban ahsante popote utakapokuwa, Ndugu Ali Hussein - Mjumbe, Ndugu Said Salim

- Mjumbe, Ndugu Mwanajuma Makame - Mjumbe ahsante, Ndugu Saada Mwenda ahsante, Iakini pia Makatibu Ndugu Aziza Kheir, Mwaka Waziri na Salim Suleiman karibuni sana Wajumbe wa Kamati ya Viwanda kutoka Baraza la Wawakilishi. Tunafarijika sana kila mnapotutembelea hapa Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge amba ni wawakilishi wa KAKEHASHI Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Nicholas Nderungo Mwenyekiti wa KAKEHASHI Tanzania karibu popote ulipo pamoja na Ndugu Henry Miku ambae ni Katibu wa KAKEHASHI karibu sana. Wageni Wanne wa Mheshimiwa Rashid Shangazi amba ni wafanyakazi wa *Clouds Media Group* kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Adam Mchomvu karibuni sana *Clouds*.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni Watatu wa Mheshimiwa Yahya Khamis amba ni jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Serge Menye karibuni sana naona wapo njiani bado hawajafika. Wageni 10 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde na Mheshimiwa Sylvia Sigula amba ni wasanii wa muziki wa kizazi kipywa wanaokuja kwenye tamasha la muziki la “/am Marioo”. Eeeh hatari hiyo wapo pale! kutoka Dar es Salaam sijui tafsiri yake ni nini mtu kuwa Marioo.

Wawakilishi Watatu wa kampuni ya *Longrich* inayojishughulisha na utengenezaji wa virutubisho na bidhaa za matumizi ya chakula lishe (*Food Supplements*) Ndugu Paschalia Funga karibu haya huyo hapo wanaopenda *Supplements* hapo. Wageni Wawili amba ni mratibu wa ofisi ya Mufti Tanzania Makao Makuu Dodoma Ndugu Al-Haji Sheikh Swed Twaibu, ahsante nakuona karibu sana, yupo na Ndugu Othman Hotty Mratibu wa Kanda ya Kati chini ya BAKWATA *Online Academy* ahsanteni sana, nawashukuruni sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja. Nawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kutakuwa

na michezo ya Mabunge ya Afrika ya Mashariki, michezo hii itaanza tarehe Nne hadi tarehe 18 Disemba Jijini Arusha. Kutakuwa na uwakilishi mkubwa nadhani watumishi na wafanyakazi hawatapungua 130 kutoka Bunge hili, lakini kama unajua nchi Jirani za Kenya na Uganda wao wanakuja hata 300 wanafika, kwa hiyo wanatufunika pale uwanjani maana wamejaa wao. Kwa hiyo Wabunge ambao mtakuwa mitaa ya Arusha, Moshi na Kaskazini ya nchi tafadhalini tarehe hizo tafuteni siku moja moja za kufika na kushangilia timu zetu. Michezo hii lengo lake ni kujenga urafiki, undugu kufahamiana katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Watakuwepo Wabunge wa Burundi, Wabunge wa Rwanda, Wabunge wa Sudan Kusini, Uganda, Kenya na wenyewe Tanzania. tunaitakia kila la kheri timu yetu ya michezo mbalimbali ambayo itashiriki wakiwemo wa *football*, watakuwepo wa *netball*, watakuwepo wa *basketball*, watakuwepo wa *volleyball*, watakuwepo riadha ikiwepo na kutembea watakuwepo wachezaji wa *golf* watakuwepo wachezaji *darts* na bila ya kusahau watakuwepo wa kuvuta kamba. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hebu wale wa mchezo wa kuvuta kamba wasimame baadhi yao ambao wapo hapa, wavuta kamba wote wasimame, eeh nafikiri mnaona, naomba tuishangilie timu yetu ya kuvuta kamba, ahsanteni sana. Wale Waganda na Wakenya wajiandae kwenye kamba safari hii na Spika nitakuwepo siku hiyo pale timu yangu mkivutwa, nitakuwa nimeanguka maana yake nitakuwa kantini yangu ya Bunge haina lishe ya kutosha. Tunatarajia michezo ya kirafiki lakini tunategemea tuchukue makombe yote kwa sababu inafanyika hapa nyumbani. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, aidha timu ya Bunge ya michezo yote hiyo itaingia kambini kuanzia tarehe 21 Novemba mwaka huu. Majina ya watakaoshiriki tutawasiliana moja kwa moja bado yanafanyiwa kazi hivi sasa, tunajaribu kuangalia bajeti yetu na hali halisi lakini tutajitahidi kadri Mungu atakavyotujalia, ashante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilisikia mwongozo watu wawili, tuanze na Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako kwa mujibu ya Kanuni ya 53 (1)

SPIKA: Kanuni ya 53?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Ndiyo.

SPIKA: Ngoja niweke mambo yangu sawa sawa hapa na wewe ufungue utusomee ili tuende pamoja, siyo kila mtu ana Kanuni humu ndani. Haya mimi nimeshafikia hapo endelea.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, inahu maswali kutokujibiwa kikamilifu. Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama ilivyoulizwa isipokuwa kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi au Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza au kabla ya muda wa kujibowi swali hilo haujafikiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati nauliza maswali yangu mawili, swali la kwanza ambalo lilihusu mkakati wa Serikali wa kuhakikisha unaratibu takwimu za ukatili dhidi ya watoto kutoka kwenye vyote na nikataja, sasa hivi swali alilojibu alionesa tu kwamba chanzo alichokipata ni cha Polisi lakini kasema hata Ustawi wa Jamii wana *source* ambazo zinaweza kuonesha takwimu za ukatili wa kijinsia, nikataja pia Kamati ya MTAKUWWA, nikataja pia mashirika yasiyo ya Serikali, lakini nikataja pia kuna mambo ya ukatili wa kijinsia yanatokea lakini kuna familia zinamalizana chini kwa chini, kwa hiyo wakienda hata akienda kwa Wenyeviti wa Mitaa au wa Vijiji wangeweza kupata hizi takwimu.

Mheshimiwa Spika, sasa nikataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, wanaratibu upatikanaji halsia wa ukatili wa kijinsia. Wakati Mheshimiwa Waziri wa

nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anajitahidi kujibu hapa swalii akataja bayana kwamba, swalii la kwanza la mkakati wa takwimu atalijibu Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, lakini alipopewa fursa ya kujibu akasema hana chakusema.

Mheshimiwa Spika, sasa ningetaka kujua Mwongozo wako, hili swalii la msingi sana ambalo litatupa uhalisya wa takwimu za ukatili dhidi ya watoto tutajibowi lini na Serikali kwa manufaa ya Watanzania, hasa hawa watoto? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana swalii lile la nyongeza lilikuwa na mambo mengi yamewekwa kwa pamoa ambayo yanahitaji takwimu na yanahitaji mambo mengi na ukizingatia kwamba, lilikuwa ni swalii la nyongeza. Swalii la namna hiyo kama linakuwa ni swalii la msingi ni rahisi sana mtu anayejibu swalii akaja na hizo takwimu za *data* na namba wakati anapoandaa majibu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, isiwe shida kwa sababu, takwimu zote ambazo zinahitaji *data* na mambo mengine yote kama zina *interest* ya Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla sisi kama Serikali tuko tayari tu. Tunao uwezo kabisa wa kuziandaa hizo *data* na kuzileta ndani ya Bunge na zikaweza kufahamika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati tumemueleza hapa, tunamaliza mkakati wa kwanza na sasa hivi ndio tunaufanya *review*, lakini tutakapokuja na mkakati wa pili, mapungufu yaliyojitokeza kwenye mkakati wa kwanza yatazingatiwa kwenye mkakati wa pili, kwa hiyo, kila jambo litazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Esther hata hivyo sisi Serikali muda wote tuko kazini, hata baada ya Bunge hili tunao uwezo tu Mheshimiwa Esther tunakualika, tuna uwezo kabisa tukakaa, tukazungumza yale maeneo ambayo

unaona ungependa yafayiwe kazi kwa haraka tutaya fanyia kazi. Lakini kama ni kwa *interest* ya Taifa kwa utaratibu mwingine wowote hata kama swali litaulizwa na Mbunge mwingine tuko tayari tuna uwezo wa kusema hayo, ili mradi tu mtu anayetaka swali la *data* atuletee mapema tuijandae na tuweze kulisema. Lakini kwenye maswali ya nyongeza ni kazi ngumu kuwa na *data* kwenye maswali ya nyongeza. (*Makofi*)

SPIKA: Basi na mimi huo ndio Mwongozo wangu. Na kama hujaridhika sana basi litunge tena swali hilo katika namna ya aina ya *data* unazozihitaji tutalipanga safari ijayo. Mwongozo unaofuata, Mheshimiwa Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kusoma Kanuni ya 54(1).

SPIKA: Subiri kidogo ili twende pamoja. Mheshimiwa Maganga leo mtaalam wa kanuni, mtani wangu. Tuendelee Mheshimiwa Maganga tafadhali. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nisome, Kanuni ya 54(1) inasema; "*Baada ya muda wa maswali kwisha Mbunge ye yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye orodha ya shughuli za ...*" (*Kicheko*)

Aah, msicheke Waheshimiwa Wabunge, msicheke naomba kabisa niko *serious* na nina hasira, tatizo nikiwa na hasira huwa nashindwa kufanua masuala. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde. Naomba unilinde.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge namlinda Mheshimiwa maganga, tafadhali.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, na ninahisi sasa... (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Nimeshakuelewa.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, na ninahisi hii ni hatua ya mwisho sasa niseme ninasema kabisa yani kwa dhati kwa moyo wangu mmoja, sijachanganyikiwa wala sjalewa.

“...kuahirisha shughuli za Bunge, ili kujadili jambo la dharura.”

Mheshimiwa Spika, jimboni kwangu leo usiku limetokea jambo la dharura, wananchi wangu wamevamiwa na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa majina naitwa Nicodemus Henry Maganga, ni Msukuma. Ni Msukuma ambaye aliyeeelimika, nina hasira sana pale ninapoona wananchi wangu wanavamiwa kwenye maeneo yao. Nimehanganya na jambo hili ni takribani sasa mwezi mmoja na wiki mbili nikitafuta hatma ya wananchi wangu maana wamekuwa wakivamiwa. Baada ya kufa Hayati Magufuli, Jimbo la Mbogwe lilivamiwa na leseni zisizojulikana, leseni hizo zilikuwa zikitoka kwa ukiukwaji wa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, na ninaomba univumilie sana na unisaidie, moyo wangu umeumia sana, nimeitwa kichaa. Na ninasema leo Bunge linafungwa ninarudi nyumbani Mbogwe migodi yangu ya Mbogwe yote naifahamu, nataka niseme kwa mara ya mwisho kama hamtanisaidia Waheshimiwa Wabunge, waliovamia migodi ya Jimbo langu la Mbogwe ama zangu ama zao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, na mimi nataka niseme, mimi huwa ninasali. Huwa namuabudu Mungu katika roho na kweli. Siwezi kuzungumza sehemu yoyote kitu ambacho sina uhakika nacho. Nimezaliwa mwaka 1980 katika Kijiji cha Mpakali, nina akili timamu, sijawahi kufeli mtihani wowote ule katika Shule ya Msingi Ningwiza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde ili nitoe ukali...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Maganga ngoja nikulinde zaidi. Waheshimiwa Wabunge ...

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: ... ili nitoe maneno yangu makali nisije nikaenda huko nikauwa watu...

SPIKA: Subiri kidogo Mheshimiwa Maganga. Waheshimiwa huwa kuna mambo baadhi yake ni *very serious*, mojawapo ni hili. Ukimuona mtu yuko kwenye *state of mind* ya namna ile tumpe nafasi aseme kwa sababu, tunaweza kukutana siku nyingine hapa tukajuta sote.

Mheshimiwa Maganga nakupa nafasi.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, siumwi, na kama ninaumwa hapa Bunge kuna hospitali tunaweza tukapima vipimo vyote maana kumekuwa na *challenge* kila nikizungumzia suala hili kuna watu ambao ni wasaliti wanaleta kanuni ambazo ni za kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme nasali na niliapa hapa Bungeni kwa mujibu wa Katiba hiyo kwamba nitailinda, lakini nitamtunza Rais wangu. Hata juzi pale Ikulu nilionesha vitu vya ajabu sana kumbe sikujua kama kuna utaratibu fulani; mimi nimepewa na Mheshimiwa Rais nizungumze wa kwanza na nilionekana wa ajabu sana...

SPIKA: Turudi kwenye hoja yako ni nini hasa?

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, hoja yangu nataka nielimishwe kwa nini wananchi wangu wamekufa mpaka sasa hivi sita, ambapo walikuwa wanadai haki yao kupitia Mahakama ya Shinyanga imekuwa ikitoa hukumu kinyume cha sheria ambalo ni kosa la jinai kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuna hukumu karibia tatu ambazo zimetoka zimesababisha wananchi wangu wafe, akiwemo binamu yangu. Nimeshawishiwa, nisinge kuwa na pesa ningepokea rushwa, nafsi yangu haki ya Mungu, baba yangu mzazi Henry Maganga ningepokea hela, lakini nashindwa

kuthamanisha ndugu yangu aliyeuwawa kikatili na watu wa madini wakijitambulisha wao ni maafisa usalama wako kwenye *system*. Na nimekuwa nikiwasiliana na ndugu zangu walioko kwenye *system* ninaona kabisa hapa hakuna haki.

Mheshimiwa Spika, naomba nikomee hapo, ili Wabunge wajadili. Mkiona kwamba, suala hili ni la mzaha ...

WABUNGE FULANI: Toa hoja.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, hoja yangu naomba Bunge lijadili jambo hili maana ...

WABUNGE: Toa hoja!

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ni mgeni naomba kuelimishwa ndugu zangu.

WABUNGE: Toa hoja.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, haya natoa hoja, naomba niungwe mkono. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Mimi nilivyoangalia jambo hili nimeona limeungwa mkono kweli kweli na utaratibu wote umefuatwa, lakini tutajadili nini jamani? Kwa sababu, ni jambo zito, sio kwamba tungemuwekea *appointment* Mheshimiwa aonane na Waziri Mkuu baadaye? Na labda, Mheshimiwa Lusinde au nani? Unataka kutoa ushauri? Haya bwana. (*Makofi*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ushauri kwa sababu, jambo hili amekuwa akililalamikia Mheshimiwa Mbunge. Ningeshauri pengine badala ya kumruhusu Mbunge akutane na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini pengine Bunge lingeunda tume ndogo, ikaenda kujiridhisha malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge halafu ndio tukaja kupata nafasi ya kujadili huko mbele ya safari, ahsante.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, tunalionia hili jambo na kama ulivyosema na alivyosema Mheshimiwa Lusinde kwamba ni jambo ambalo liko kidogo linatakiwa kuli-*handle* kwa utaratibu fulani. Lakini kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameeleza hapa mambo fulani mazito ya namna moja ama nyingine wakati tunajiandaa kutafuta njia nzuri ya kulishughulikia, kama Kiti chako kitaturidhia Serikali labda Mheshimiwa Waziri wa Madini angesema kidogo sana halafu tupate nafasi ya kuweka utaratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, ninakuomba sana kwa sababu, Serikali iko kwa ajili ya kulinda wananchi. Angalau kwa dakika chache tu, kama itakupendeza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)

SPIKA: Sina tatizo katika hilo, lakini busara yangu inaniambia lisiende hivyo. Kwa sababu, kama ambavyo mmemuona Mheshimiwa na alishafika mpaka kule, na kadhalika na hawa ni majirani, yaani Jimbo lile pale Mbogwe na Bukombe ni majirani kabisa. (*Makofi*)

Ni kwamba huku kuna Mbunge huku kuna Waziri na mambo hayo ndio hayo mpaka na mauwaji na nini yanavyosemwa na kadhalika ilihitajia mtu wa ngazi ya juu kidogo ili sasa yeye, kama hivi Waziri Mkuu akimuita Waziri wake na yule mlalamikaji, yaani pakawa na mtu wa tatu, lakini likifanyika la watu wawili linakuwa kidogo kama vile tabu. (*Makofi*)

Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu kwa wakati wako umpate Mheshimiwa umskilize na kwa busara yako sisi tunakuaminia kabisa kama Mkuu wa Shughuli za Serikali

Bungeni ili kuona namna gani jambo hili likoje liweze kuwekwa vizuri. (*Makofi*)

Makofi haya maana yake mmetukubalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Maganga na wewe nakuomba unikubalie kwa hatua hizi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali hebu ashughulike na hili kwanza. Waheshimiwa nawashukuruni sana.

Katibu!

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo 9 kwa Lengo la Kuondoa Upungufu Aambao Umejitokeza katika Sheria hizo Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria Hizo. [*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Law Updated with some Challenges Observed in its Implementation*].

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.7) wa Mwaka 2021 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Bill, 2021].

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

SPIKA: Ahsante sana. Basi kuna Muswada huo wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 7) wa Mwaka 2021, umeshasomwa mara ya kwanza. Na kwa hiyo, Muswada huo naupeleka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria muanze kujipanga, ili muweze kuupitia na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu utakuwa kwenye mitandao na vishikwambi vyenu baada tu ya kuwa umesomwa mara ya kwanza na ninyi mnapoenda majimboni basi muanze kupitia

kuona kuna nini katika Muswada huo, ili tutakaporudi basi tuende na muswada huu katika hatua zake zinazofuata.

Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

SPIKA: Katibu wa Bunge.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa Taarifa kwamba, shughuli zote zilizowekwa kwenye orodha ya shughuli za Mkutano wa Tano wa Bunge, sasa zimemalizika.

SPIKA: Kwa kuwa, shughuli zote zimekamilika sasa kama ilivyopangwa, na hii inaonesha jinsi gani ambavyo Bunge ni moja ya taasisi za Serikali ambazo ni *extremely efficient*. Kwamba, tukipanga shughuli zetu kwamba, zinaanza hapa zinaishia hapa, zinaishia palepale. (*Makof/ Kicheko*)

Basi, kwa vile zimekamilika kama ratiba yetu ilivyokuwa tulivyoambiana siku ya *briefing*, katibu sasa nakuita kwa shughuli inayofuata.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Hoja ya Kuahirisha Bunge. Sasa naomba moja kwa moja nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, ili awe ni Mtoa Hoja ya kuahirisha Bunge kwa kadiri ya Kanuni yetu ya 35(3). Mheshimiwa Waziri Mkuu nakukaribisha hapo mbele. Karibu sana kwa hotuba yako. (*Makof/*)

WAZIRI WA MKUU: Mheshimiwa Spika, leo hii tunafikia tamati ya Mkutano wa Tano wa Bunge lako Tukufu ulioanza

tarehe 02 Novemba, 2021. Kwa msingi huo tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa Rehema kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye mkutano huu tukiwa buheri wa afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa weledi, busara na uwezo mkubwa uliouonesha katika kuliongoza Bunge hili umekuwa chachu ya kuhitimisha shughuli za Bunge hili kwa mafanikio makubwa. Hivyo, basi nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitakushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa umakini mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kutusaidia kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu tukufu. Niwashukuru pia, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi nzuri, michango, maoni na ushauri tuliopokea katika mkutano huu. Serikali kwa upande wake imepokea michango yenu yenye nia ya kujenga na kuimarisha utendaji wa Serikali na ninaahidi kwamba, michango yote na ushauri wote tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Septemba, 2021 Bunge lako tukufu lilipata pigo kubwa kwa kuondokewa na Mheshimiwa William Tate Olenasha, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na aliyekuwa Naibu Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji. Ninatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Ngorongoro na Wilaya ya Ngorongoro, Ndugu jamaa na marafiki wote walioguswa na msiba ule.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika katika kipindi hicho cha Septemba hadi Novemba, 2021 wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na masahibu mbalimbali ikiwemo ajali za barabarani ambazo zimegharimu maisha ya watu, majeruhi na kusababisha uharibifu wa mali. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema na awaponye majeruhi wote waliohusika kwenye ajali mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Septemba, 2021 vilevile Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri ambapo alimteuwa Mheshimiwa Dkt. Stegomena Laurance Taksi, Mbunge, kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pia, alimteuwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge, kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Pia, alimteuwa Mheshimiwa January Yussuf Makamba, Mbunge, kuwa Waziri wa Nishati. Pia, alimteuwa Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na pia, Mheshimiwa Dkt. Alieza Mbuki Feleshi, kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwatakia heri katika kutimiza majukumu yao viongozi wote wallioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali. Niwakumbushe tu kwamba, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo matarajio makubwa kutoka kwenu katika kutimiza shahuku ya Watanzania kuona mafanikio kwenye sekta mnazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu jumla ya maswali 98 ya msingi na mengine 247 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali nane ya papo kwa papo yalielekezwa kwa Waziri Mkuu na kujibiwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lilipokea na kujadili Taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Tatu, tarehe 9 Aprili, 2021 na Mkutano wa Nne, tarehe 7 Septemba, 2021 pamoja na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, tunapohitimisha Mkutano huu, tumeweza kukamilisha mjadala wa Miswada miwili ya sheria iliyyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2021 ulisomwa kwa hatua zake zote na Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.7 wa Mwaka 2021 ulisomwa pia kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Mbili, Serikali iliahidi kuwasilisha Muswada wa Sheria kuhusu Bima ya Afya kwa Wote. Serikali inatoa umuhimu mkubwa kwenye suala hili sambamba na kuhakikisha masuala yote ya kisera, kisheria na kibajeti yanatazamwa kwa kina. Hatua muhimu za awali zimekamika na sasa tunawashirikisha wadau wengi zaidi ili kutengeneza mfumo ambao hautokuwa na changamoto nydingi.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuona utekelezaji wake unaanza mwaka ujao wa fedha 2022/2023 ili kila mwananchi awe na uhakika wa kupata matibabu kila inampolazimu. Hivyo basi, nitoe maelekezo kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kushirikiana na wadau wote muhimu katika kuhakikisha Muswada wa Sheria kuhusu Bima ya Afya kwa Wote unakamilika kwa wakati ili kukidhi malengo ya Serikali na matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Oktoba mwaka huu 2021, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 hapa Jijini Dodoma. Mpango huo uliotokana na mkopo nafuu wa takriban shilingi trillioni 1.3 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (*IMF*) unaolenga kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukabiliana na athari za UVIKO19 katika uchumi na maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sekta zitakazonufaika na mpango huo ni Sekta ya Maji imepata (shilingi bilioni 139.4), Sekta ya Elimu (shilingi bilioni 368.9), Sekta ya Afya (shilingi bilioni 466.9), Sekta ya Utalii (shilingi billioni 90.2), Jamii inayoishi kwenye mazingira magumu nayo itanufaika kwa (shilingi bilioni 5.5) zikiwemo kaya maskini na Kundu la Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu ambao pia wametengewa (shilingi

bilioni 5.0). Aidha, shilingi bilioni 231 zimeelekezwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi bilioni 5.0 ni kwa ajili ya shughuli za uratibu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huo utaimarisha miundombinu ya afya, elimu, maji, utalii na maeneo ya biashara za wajasiriamali wadogo, uwezeshaji wa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na kaya maskini. Kwa upande mwingine, mpango huo utaimarisha upatikanaji sambamba na kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi. Hii inatokana na ukweli kwamba uwekezaji mkubwa umefanywa kwenye eneo la vifaa hususan mitambo ya uchimbaji wa maji na visima na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo za dharura zitapaswa kutumika ndani ya kipindi cha mlezi tisa hususan mwaka huu wa fedha 2021/2022. Kwa kuzingatia hilo, Serikali tayari imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha matarajio ya Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa mpango huu yanafikiwa. Baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuunda Kamati za Uratibu kwa ngazi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kila mkoa na halmashauri ambapo Kamati hizi zimejumuisha viongozi kutoka ngazi ya Wizara, Wakuu wa Idara na Vitengo watakaokuwa na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa miradi yote iliyoainishwa.

(ii) Kuandaa utaratibu wa manunuzi ya pamoja kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa vifaa vya huduma za dharura, *ICU*, *X-Ray*, magari ya kubebea wagonjwa ambayo yatagawiwa katika Halmashauri zote nchini na magari ya uratibu wa huduma za afya katika mikoa yote;

(iii) Kuwaelekeza Wakuu wote wa Mikoa, Wilaya na Watendaji wa Halmashauri kuepuka safari zisizokuwa za lazima katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango huu wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19; na

(iv) Kuhamasisha wananchi na wawakilishi wao kushiriki ipasavyo katika ujenzi wa miradi inayoendelea kwenye maeneo yao na kutoa taarifa endapo watabaini uwepo wa viashiria vya ubadhirifu wa fedha au vifaa vya miradi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo na katika kuhakikisha uwepo wa thamani ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo, naelekeza masuala yafuatayo kwa wote wanaohusika:-

(i) Viongozi na Watendaji wasimamie na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi yote iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19

(ii) Wakuu wa Mikoa wote, Makatibu Tawala na Wakuu wa Wilaya wahakikishe hadi kufikia Januari 2022, madarasa yote kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza yawe yamekamilika; (*Makof*)

(iii) Wakuu wa Mikoa wahakikishe wanasmamia ipasavyo mipango ya usimamizi kuititia Sekretarieti za Mikoa. Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa nazo zihakikishe kwamba zinafuatilia utekelezaji huo sambamba na kutembelea maeneo husika ili kujiridhisha hasa kwenye thamani ya fedha na ujenzi unaofanywa kwenye maeneo husika.

(iv) Lakini mwisho Wakuu wa Mikoa wahakikishe kwamba Sekretarieti husika zinashirikisha wananchi sambamba na wawakilishi wao katika kutekeleza miradi iliyopo kuititia Mpango huu wa UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba ilikuwepo hofu kuhususia kupatikana na wakati mwingine kupanda kwa bei ya baadhi ya vifaa vya ujenzi ikiwemo saruji, batii, nondo, marumaru, vifaa vya umeme na kadhalika. Katika hatua ya kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilikutana na wazalishaji na hata kutembelea baadhi ya maeneo ya

uzalishaji ili kujiridhisha kuona hali ilivyo kwa upande wa bidhaa hizo kuwa zinapatikana tena kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba wazalishaji wetu wamejipanga vizuri kuzalishaji na hatutarajii uhaba au mtikisiko wa bei kwa bidhaa lengwa. Niendelee kusisitiza kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara isimamie na ifuatilie mwenendo wa bei ya bidhaa hizi kutoka viwandani bila ya kupanda kutokana na mkakati huo wa ujenzi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia lilipokea na kujadili, ushauri na kupitisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika kukidhi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3)(c) na Kanuni ya Kudumu za Bunge lako Tukufu Ibara ya 11, hoja hiyo ilijadiliwa kwa siku tano kuanzia tarehe 3 Novemba, 2021 na kuhitimishwa tarehe 9 Novemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yao kwa maelezo mazuri ya ufanuzi waliyotoa wakati wa kuhitimisha hoja yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa mchango wao mzuri waliyotoa wakati wa mjadala wa hoja hiyo. Katika mjadala ule, tulipata darasa zuri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wametupa uelewa mpana utakaotusaidia kuboresha utekelezaji wa mpango huo kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 ni wa kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka 2022/2023, Mpango huo utaendelea kutekeleza maeneo mahsusini ya kipaumbele ambayo ni:

- (i) Kuchochera uchumi shindani na shirikishi;
- (ii) Kuimarisha uwezo wauzalishaji viwandani na utoaji huduma;
- (iii) Kukuza biashara na uwekezaji;
- (iv) Kuchochera maendeleo ya watu; na
- (v) Kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mapendekezo ya Mpango huo, pia uliwasilishwa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023. Hivyo, nami nitumie fursa hii kusitiza baadhi ya mambo muhimu ambayo hayana budi kuzingatiwa na viongozi watendaji wote wakati wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 kama ifuatavyo:-

- (i) Suala la ukusanyaji wa Mapato ya Ndani. Hili ni mionganini mwa maeneo yaliyoibua hoja kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Hivyo, nisilitize kuwa Wizara ya Fedha ishirikiane na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuimarisha matumizi ya vifaa vya kielektroniki katika kukusanya mapato ya ndani ya Serikali;
- (ii) Suala la riba kubwa za mikopo kutoka kwenye mabenki ya biashara na taasisi za fedha. Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti kuititia Benki Kuu ya Tanzania ikiwemo kupunguza kiwango cha akiba kinachowekwa na mabenki katika Benki Kuu, lakini pia kulegeza masharti ya uanzishwaji wa Ofisi za Wakala wa Mabenki, kushusha riba inayolipwa kwa akaunti za fedha za mitandao pamoja na kutenga shilingi trilioni moja kwa ajili ya mikopo kama benki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia tatu ili mabenki na taasisi hizo zitoe mikopo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zinalenga kupunguza kiwango cha riba kwenye mikopo ya mabenki ya kibiashara na taasisi za fedha; kupunguza riba pia katika shughuli za kilimo kwa kiwango kisichozidi asilimia 10; na kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi ili kuchechemua shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, licha ya hatua hizo, bado kumekuwa na changamoto ya kutoshuka kwa kiwango cha riba kitakachotozwa na mabenki na taasisi za fedha. Kwa mantiki hiyo, naiagiza Wizara ya Fedha na Mipango ikutane na taasisi za fedha nchini kuona namna watakavyoweza kupunguza riba kubwa kwenye mikopo wanayotoa hususan kwa makundi ya wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo;

(iii) Kuwawezesha Wakandarasi wa Ndani: Wizara ya Fedha shirkianeni na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika kuhakikisha kwamba inatekeleza vema Mpango wa Serikali wa kuwajengea uwezo na kuwawezesha wakandarasi wa ndani sanjari na kuendelea kulipa madeni ya wazabuni kwa wakati;

(iv) Suala la Mafao ya Wastaifu. Katika hili namuelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Uratibu na Wenye Ulemavu) kushirikiana na Waziri wa Fedha na Mipango katika kuhakikisha kwamba changamoto ya upatikanaji wa mafao ya wastaifu kwa wakati inaondoka na wastaifu walipwe kwa wakati;

(v) Kudhibiti Matumizi na Kupunguza Gharama: Maafisa Masuuli endeleeni kuchukua hatua za kupunguza matumizi yasiyokuwa na lazima na kuhakikisha kuwa taasisi za Serikali zinazojiedhesha kibiashara, zinapata faida na kuacha kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu.

(vi) Kudhibiti Ongezeko la Madeni ya Serikali: Maafisa Masuuli wote hakikisheni madai ya watoa huduma yote yanahakikiwa na kuingizwa kwenye hesabu za fungu husika, kutoingia mikataba ya miradi mipya bila kuwa na uhakika wa upatikanaji fedha na kuzingatia matumizi ya hati za

ununuzi zinazotolewa kwenye mfumo wa malipo ili kudhibiti ulimbikizaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwakumbusha viongozi na watendaji wote Serikalini kuzingatia kikamilifu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2022/2023 ili kuendeleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo; uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2020/2021 ulikuwa mzuri. Katika msimu huo uzalishaji ulifikia tani milioni 18.42 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 14.79. Kwa lugha nyingine tuna ziada ya tani milioni 3.63.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tupo katika msimu wa kilimo 2021/2022, ambapo baadhi ya maeneo ya nchi yetu yameanza kupata mvua za vuli. Hata hivyo, taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania iliyotolewa Septemba na Oktoba, 2021 imeonyesha kuwa viwango vya unyeshaji mvua katika msimu huu wa kilimo vitakuwa vya wastani katika baadhi ya maeneo hali imbayo itaathiri uzalishaji wa baadhi ya mazao kama mpunga na mahindi kutokana na vipindi virefu vya ukame.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshachukua hatua mahsusili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na upungufu wa mvua. Hatua hizo ni pamoja na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuendelea kununua chakula na kuhifadhi. Serikali itafuatilia kwa karibu mwenendo wa ukuaji wa mazao shambani sambamba na kufanya tathmini ya hali ya hewa, lakini pia na hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanaji wa Mbola; ni dhahiri kuwa matumizi ya mbola, mbegu bora na viuatalifu ni muhimu katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika kuzalisha, kuagiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima kulingana na mahitaji na ikolojia ya kilimo. Serikali imekuwa

ikichukua hatua kadhaa katika kuhakikisha pembejeo za kilimo hususan mbolea zinapatikana kwa bei nafuu, kwa wakati, lakini pia kwa kiwango cha kutosha. Miongoni mwa hatua hizo ni matumizi ya mifumo ya upatikanaji wa mbolea kuititia uzalishaji ndani na uagizaji wa mbolea kutoka nje pamoja na kuruhusu mbolea kuingia kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2021/2022, makisio yanaonyesha kuwa mahitaji ya mbolea ni tani 698,260 na wastani wa matumizi kwa mwaka ni tani 430,000. Hata hivyo, hadi kufikia Oktoba, 2021, upatikanaji wa mbolea ulikuwa ni tani 333,903 sawa na asilimia 48 tu ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa mbolea duniani kote imeathiriwa na uwepo wa UVIKO 19. Hali hiyo, imesababisha kusimama kwa uzalishaji, baadhi ya nchi kusitisha uuzajji wa mbolea nje ya nchi, lakini pia kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na upungufu wa malighafi za kutengenezea mbolea kutokana na baadhi ya nchi kufunga mipaka yake na hivyo kusababisha ongezeko la mahitaji na bei kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kusuasua kwa uagizaji wa mbolea na ongezeko la bei kwa takribani asilimia 96 ikilinganishwa na bei ya mwaka jana, Serikali imechukua hatua za haraka kukabiliana na hali hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Kuwasiliana moja kwa moja na wazalishaji wa mbolea katika nchi rafiki ili kupata mbolea kwa gharama nafuu;

(ii) Kuruhusu wafanyabiashara kuingiza mbolea nchini bila kutumia zabuni za mfumo wa ununuzi wa pamoja na kuuza kwa bei ya ushindani. Hatua hii imesaidia kuongeza kiwango cha mbolea kilichoingizwa nchini kati ya Julai na Oktoba, 2021. Katika kipindi hicho, tani 48,400 za mbolea ya *Urea* ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 33,948 zilizonunuliwa kwa zabuni ya mfumo wa pamoja msimu kwa 2020/2021;

(iii) Kuhamasisha matumizi ya mbolea mbadala wa *DAP* na *Urea* kama vile *NPK*, *NPS*, *NPS Zinc*, pamoja na Nafaka+ inayotengenezwa Minjingu, mbolea za asili, chokaa na mbolea ya *Fomi Imbura* inayozalishwa na Kiwanda cha Fomi cha Burundi;

(iv) Kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea ikiwa ni sehemu ya suluhisho la muda mrefu. Tayari ujenzi wa kiwanda cha Kampuni ya *Itracom Fertilizers Limited* kutoka Burundi umeanza na utakapokamilika kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka. Kadhalika, kuongeza uzalishaji katika kiwanda cha Minjingu ili izalishe sawa na uwezo wake wa tani 100,000 kwa mwaka;

(v) Kukamilisha mazungumzo na Serikali ya Burundi kuhusu kununua mbolea ya *Fomi Imbura*. Nitoe wito kwa Watanzania kuendelea kuzitumia aina nyngine za mbolea kwani pia zinaweza zinatumika kwa mafanikio kwa nchi jirani na hata baadhi ya maeneo hapa nchini.

(vi) Serikali kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania (*TFC*) imekwishaagiza tani 20,000 za mbolea ya kupandia (*DAP*) na tani 60,000 za mbolea ya kukuzia (*Urea*). Mbolea hii itauzwa kwa gharama nafuu ambayo inalingana na uwezo wa wakulima wetu hapa nchini;

(vii) Kukamilisha utafiti wa afya ya udongo katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Tanga, Ruvuma, Tabora na Kigoma kwa lengo la kuwezesha viwanda vya mbolea hususan vilivyoko nchini kuzalisha mbolea kulingana na afya ya udongo sambamba na matumizi sahihi ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa taarifa muhimu na elimu kwa Umma kuhusu hali ya hewa na bei ya mbolea duniani. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mnaporudi kwenye Majimbo yetu tutoe taarifa na tutoe elimu kwa wananchi kuhusu changamoto inayotukabili hasa kwenye sekta ya mbolea na hususan

kuhamasisha matumizi ya mbolea mbadala zinazopatikana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza Wakuu wa Mikoa wote nchini na hasa wanaokaa mikoa ya mipakani kutozua mbolea inayoingia ndani ya nchi kwa namna yoyote ile. Mahitaji yetu ni kupata mbolea, lakini pia hatutaruhusu kutoa mbolea ndani ya nchi kwenda nchi nyngine kwa sababu mbolea tuliyonayo nchini haitoshi kwa matumizi ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Taifa letu lina mfumo wa umwagiliaji wenyewe ukubwa wa hekta 600,000 ambapo mtandao huo pamoja na uwepo wake haufanyi kazi kwa asilimia 100. Kwa kuzingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba Sekta ya Umwagiliaji inakua na miundombinu ya umwagiliaji yenyewe ukubwa wa hekta milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025. Nawaagiza Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha kukaa pamoja na kufanya mambo yafuatayo kwenye Mpango wa Mwaka 2022/2023 hasa kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha:-

(1) Mhakikishe kwamba kila Mkoa na Wilaya kuna Ofisi ya Tume ya Umwagiliaji na vitendea kazi vinakuwepo na *ma-engineer* wenyewe sifa;

(2) Kuhakikisha kuwa *ma-engineer* wa umwagiliaji waliopo kwenye Halmashauri na *ma-engineer* wa Tume ya Umwagiliaji wanafanya kazi chini ya Ofisi ya Tume ya Umwagiliaji ili kufanya kazi kwa pamoja;

(3) Kufanya usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji kwa maeneo mapya ili kujenga skimu zenye ukubwa unaofanana, ukubwa kama ambao tumeupata ifikapo mwaka 2025;

(4) Kufanya tathimini ya kina kwa skimu za umwagiliaji zilizopo na kuzikarabati ili ziweze kufikia ubora na ufanisi unaotakiwa;

(5) Kutenga fedha kupitia bajeti ya Wizara kwa ajili ya kununua vifaa na mitambo ambayo itakuwa katika kanda zote nane za kilimo ili kutumika kwa ajili ya kutunza, kurekebisha na kujenga mabwawa madogo kwenye maeneo ambayo wakati wa masika maji mengine huwa yanapotea bila utaratibu;

(6) Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Kilimo andaeni miradi ya kielelezo ya umwagiliaji na pia andaeni maghala ya kuwekea chakula. Pia uwekezaji kwenye maeneo hayo ya uhifadhi wa mazao ya nafaka unahitajika zaidi pamoja uhifadhi wa *horticulture*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mijadala hapa ni pamoja na suala la kuharakisha upatikanaji wa umeme vijijini. Si tu kwa umeme kufika kijijini, bali kusambazwa kwenye nyumba za wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Waziri wa Fedha na Mipango alipokuwa akiwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme hususani maeneo ya vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya vijiji 10,361 kati ya vijiji 12,317 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 84.12, vimeunganishwa na umeme. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba hadi kufikia Desemba, 2022 vijiji 1,956 vilivyosalia vinapata umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulioanza kutekelezwa mwezi Julai, mwaka huu 2021 na gharama za mradi huu ni shilingi triliuni 1.24.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha maeneo yote ya mijini na vijijini yanapata umeme wa kutosha, nafuu na uhakika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji na usambazaji umeme maeneo mbalimbali nichini. Baadhi ya miradi ya kimkakati ya uzalishaji umeme ni mradi wa kufua umeme na maji wa Julius Nyerere ule ambao utazalisha

Megawati 2,115 ambao utekelezaji wake umeshafikia asilimia 55.6 na mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo Megawati 80 uliofikia asilimia 81.2.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha mradi wa njia ya kusafirisha umeme KV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita wenye urefu wa kilomita 55. Miradi mingine ya kusafirisha umeme inayoendelea kutekelezwa ni kutoka Rusumo kwenda Nyakanazi kupitia Benaco KV220, Tabora kupitia Urambo - Nguruka hadi Kidahwe KV 132 na Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga KV132. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya Mradi wa Njia ya Kusafirishia Umeme Msongo wa KV 400 kutoka Iringa kwenda Mbeya, utakwenda mpaka Tunduma hadi Sumbawanga na Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa KV 400 kutoka pale Sumbawanga hadi Mpanda na kwenda kutokea Uvinza Mkoani Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi hii ya uzalishaji na usambazaji umeme kutawezesha maeneo yote nchini kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa na hivyo kupata huduma ya uhakika ya umeme. Jukumu la *TANESCO* ni kuhakikisha kwamba usambazaji umeme kwenye makazi ya watu unafanywa kwa kasi ili lengo la Mheshimiwa Rais la kuona kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme liweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu kwa kuongeza kiwango cha fedha za kugharamia mikopo ya elimu ya juu na hivyo kuongeza idadi ya wanufaika. Kwa mfano, mwaka wa masomo 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu ikilinganishwa na shilingi bilioni 464 zilizotumika mwaka wa fedha 2020/2021.

Vilevile, idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka 149,398 mwaka 2020/2021 hadi 170,000 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, upangaji wa mikopo unaendelea kwa kuzingatia utaratibu, sifa na vigezo vilivyowekwa. Kwa msingi huo, naelekeza kama ifuatavyo:-

(1) Waombaji wote wa mikopo hakikisheni mnakamilisha taratibu za uombaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kujisajili kwenye mfumo wa maombi ya mikopo kwa wakati. Vilevile, hakikisheni mnawasilisha taarifa sahihi ili muweze kuhudumiwa bila bughudha;

(2) Baada ya kufunguliwa kwa dirisha la rufaa, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu harakisheni mchakato wa rufaa ili wanafunzi husika waweze kupata stahiki zao, watulie na waendelee na masomo yao bila bugudha yoyote ile.

(3) Mamlaka zote za vyuo vikuu vyenye wanafunzi wanufaika na mikopo ya elimu ya juu kamilisheni na kuwasilisha taarifa za wanafunzi ili kuiwezesha Bodi ya Mikopo kuwapangia mikopo na kuhakikisha wanapokea stahiki zao kwa wakati na kupunguza usumbufu usiokuwa wa lazima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa mikopo ya elimu ya juu, Serikali imepokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuboreshwa kwa mfumo wa sasa wa mikopo ya elimu ya juu. Maoni hayo ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maoni mengine ni kutoa ruzuku badala ya mikopo kwa wanafunzi wanaosomea Shahada na Stahashada zenyе uhitaji mkubwa kitaifa na katika uzalishaji, na wale wanaotoka katika makundi yenye mahitaji maalumu. Pia kufanya mapitio ya vipengele vya mikopo ili kuangalia uwezekano wa kuainisha vipengele vya kukopeshwa na vinavyoweza kutolewa kwa ruzuku kati ya gharama za ada za mafunzo na zile za mahitaji mengine.

Mheshimiwa Spika, naielekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya mapitio upya ya mfumo wa utoaji mikopo ili kuzingatia maoni ya wadau na uzoefu wa miaka iliyopita na ije na mapendekezo kuhusu mfumo bora utakaotatua changamoto za sasa sambamba na kuimarisha kasi ya urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya marekebisho makubwa ya bandari zetu zilizopo kwenye Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Maboresho hayo, yanalenga kuongeza uwezo wa bandari zetu katika kuhudumia meli hususan za shehena na hivyo, kumudu ushindani wa kibiashara sambamba na kutumia vyema fursa ya kijigrafia katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Kimkakati wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 421 umefikia asilimia 99 na unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2021/2022. Kukamilika kwa mradi huu, kutaongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kuhudumia meli kubwa zinazohitaji kina kirefu zaidi kuliko ilivyo sasa, zenye urefu wa hadi mita 305 na uwezo wa kubeba makasha kati ya 7,000 hadi makasha 8,000.

Mheshimiwa Spika, vilevile, uwezo wa bandari hiyo wa kuhudumia shehena kubwa za mizigo utaongezeka kutoka tani milioni 16 za sasa hadi tani milioni 25. Hivyo, kuongeza mapato ya Taifa na kumudu kushindana kibishara na bandari nyiningine za ukanda wa Bahari ya Hindi kama vile Mombasa, Maputo, Beira, Nacala pamoja na Durban.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Bandari ya Dar es Salaam imeanza kupokea meli kubwa zenye uwezo wa kubeba hadi magari 6,000 pamoja na kuongeza uwezo wa kuhudumia meli kubwa hadi tatu za aina moja ya shehena kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, tuna Bandari ya Tanga. Awamu ya kwanza ya uboreshaji wa Bandari ya Tanga ambayo

ilihusisha uongezaji wa kina cha lango la bandari kutoka mita 4 hadi mita 13 na ujenzi wa gati mbili kwenye kina kirefu umekamilika na katika mwaka 2020/2021, mradi huo uligharimu shilingi bilioni 20.41.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari hiyo wenyе lengo la kuongeza kina cha gati utekelezaji wake umefikia asilimia 13. Kukamilika kwa mradi huo kutaiwezesha Bandari ya Tanga kuondokana na ghamara kubwa za kuhudumia meli nangani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari ya Mtwara, awamu ya kwanza ya ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 litakalohudumia shehena mchanganyiko umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, ukarabati wa yadi ya kuhudumia shehena kupitia ujenzi wa sakafu ngumu eneo la mita za mraba 5,600 na ukarabati wa ghalaa Na. 3 nao pia umekamilika.

Mheshimiwa Spika, maboresho hayo yanayoendelea sasa yana lengo la kuhakikisha Bandari ya Mtwara inakuwa endelevu kwa kusafirisha bidhaa na mazao yanayozalishwa Mikoa ya Kusini ikiwemo zao kuu la korosho na mazao mengine kama ufuta; na kwa sasa makaa ya mawe yanayopatikana kule ngaka. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeongeza uwezo wa Bandari ya Mtwara kuhudumia shehena ambapo kwa sasa ina uwezo wa kuhudumia tani 1,000,000 kwa mwaka ikilinganishwa na tani 400,000 za awali.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa Bandari ya Mtwara umeongeza uwezo wake na kuifanya iweze kuhudumia meli nne kwa wakati mmoja. Vilevile maeneo ya wazi ya kuhudumia na kuhifadhi shehena yaliyosakafiwa yameongezwa hadi kufikia uwezo wa kuhudumia makasha 12,950 kwa wakati mmoja. Halikadhalika, maghala ya kuhifadhi mizigo yaliyopo yana uwezo wa kuhifadhi tani mpaka 10,000 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zinazokwenda sambamba na maboresho hayo ni kupungua kwa tozo za

aridhia kwa mazao ya kilimo kutoka asilimia moja hadi asilimia 0.5 ya malipwani ikillinganishwa na bandari nyingine nchini. Vilevile kuongeza muda wa makasha tupu kukaa bandarini kutoka siku 15 na kuwa muda wa siku chache kipindi chote cha msimu wa korosho na kuongeza muda wa makasha yenye mizigo kukaa bandarini bila tozo ya kuhifadhi kutoka siku saba hadi siku 15 na kupunguza aina ya tozo za kuhudumia meli na shehena kwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, maboresho yanayoendelea katika bandari ya Mtwara ikiwemo kuweka unafuu wa gharama za kuhudumia shehena yanalenga kuongeza matumizi ya bandari hiyo hususan katika usafirishaji wa mazao ya kilimo, jasi kwa maana *gypsum*, makaa ya mawe kutoka Ruvuma sambamba na kukuza shughuli za kiuchumi katika ushoroba wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande mwingine imeendelea na uboreshaji wa bandari zilizopo kwenye maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ili ziweze kutoa huduma bora na kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa bandari mbalimbali katika Ziwa Victoria katika ujenzi wa gati, majengo ya utawala na abiria, na maghala ya kuhifadhia mizigo katika Bandari za Magarine kule Muleba, Nyamirembe -Chato, Bukoba, Kemondo Bay, pamoja na ujenzi wa gati mbili katika Bandari ya Mwigombero - Musoma na gati moja katika Bandari za Lushamba na Nkome umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ziwa Tanganyika, Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Kibirizi na Ujiji umekamilika kwa asilimia 52 na ujenzi wa Bandari ya Karema umekamilika kwa asilimia 55. Aidha, ujenzi wa miundombinu mingine ikiwemo majengo ya abiria na ghalia la kuhifadhia mizigo katika Bandari za Kasanga, Sibwesa, Kabwe, Kipiri na Lagosa Mpanda Vijijini, Kabwe kule Nkasi na Ujiji unaendelea. Kwa upande wa Ziwa Nyasa, ujenzi wa bandari na miundombinu

mingine ikiwemo majengo ya abiria na ghala la kuhifadhiya mizigo katika Bandari ya Ndumbi umefikia asilimia 82.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kuboresha miundombinu na utoaji huduma za bandari ili kuongeza chachu ya maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Hivyo basi, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na dhamira yake ya dhati ya kutuletea maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Taifa letu linaendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika fani za utamaduni, sanaa na michezo. Shughuli mbalimbali za utamaduni, sanaa na michezo zimeendelea kuling'arisha Taifa letu kwa viwango tofauti ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu unatangazwa vyema kupitia shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo matamasha ya ngoma, mavazi, vyakula vya makabila mbalimbali na kadhalika. Hivi karibuni Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo kiliendesha Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania na lilipata mafanikio makubwa na mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tulishuhudia Taasisi ya Tulia *Foundation* ya Jijini Mbeya nayo imekuwa ikiandaa Tamasha la Ngoma za Asili kila mwaka ikijumuisha ngoma za makabila yote nchini. Tunashukuru na tunawapongeza sana kwa maandalizi hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sanaa, yapo maendeleo makubwa ikiwemo kuhusisha wasanii wengi ambaao hujipatia kipato kupitia fani hiyo. Muziki wa aina zote, uchoraji, uchongaji na maendeleo ya filamu yamekuwa chachu ya kukua kwa sanaa yetu nchini. Hivi karibuni tulitembelewa na Msanii maarufu wa filamu za Kihindi Sanjay Dutt kutoka India kwa lengo la kuja kuanzisha ushirikiano na

wasanii wa filamu wa hapa Tanzania pamoja na India na pia kutangaza utalii wetu. Msanii huyo bado yuko mbugani ambako anakagua maeneo ya kupiga picha na kutengeneza filamu za mbunga zetu ili kulitangaza Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye michezo nako yako mafanikio makubwa yamefikiwa ambako michezo mbalimbali inaendelea kuchezwa. Michezo ya Mpira wa Miguu na Mpira wa Kikapu kwa sasa ipo kwenye Mashindano ya Kitaifa ambapo Kombe la Taifa la Kikapu linaendelea hapa Jijini Dodoma linaitwa *Basket Ball Taifa Cup* chini wa ufadhili wa CRDB. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mnaalikwa kushuhudia mashindano hayo yanayoendelea kwenye viwanja vya Chinangali hapa Jijini Dodoma. Timu zetu kutoka kwenye Mkoa yetu ziko Jijini Dodoma, zinashiriki kwenye kombe la Taifa la *Basket Ball*. Timu za Taifa za Mpira wa Miguu zinaendelea na mashindano kwa ngazi mbalimbali. Kwa upande wa soka, timu zetu zimekuwa zikifanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nawapongeza sana *Twiga Stars* kwa kufanikiwa kubeba kombe la COSAFA katika fainali zilizofanyika Afrika Kusini baada ya kuzifunga Afrika ya Kusini yenyewe, Zimbabwe, Botswana, Sudani, Zambia na Malawi na kuwa bigwa wa COSAFA. Tumefanikiwa kupata mchezaji bora wa mashindano hayo, dada yetu aitwaye Amina Bilali. Tunampongeza sana Amina Bilali kwa kuwa mchezaji bora kwenye mashindano ya CECAFA mwaka huu wa 2021. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Timu yetu ya Wanawake ya "Chini ya Miaka 20, imefuzu hatua ya tatu ya kucheza Kombe la Dunia. Bado hatua mbili ambazo wakishinda watacheza Kombe la Dunia. Timu hii imeshika nafasi ya tatu katika mashindano ya CECAFA Under 20. Mchezaji wetu Aisha Masaka alipata tuzo ya ufungaji bora kwa kufunga magoli saba kwenye michezo mmoja. Nazipongeza sana timu za wanawake za mpira wa miguu. Timu ya Vijana Wanaume

chini ya miaka 20 nao pia wamechukua ubingwa wa *CECAFA* Wanaume kwa kuifunga Congo goli moja.

Mheshimiwa Spika, timu yetu ya Wanaume *Taifa Stars* inayoendelea na mashindano ya kufuzu hatua za awali za Kombe la Dunia imeondoka leo nchini kwenda Madagascar kwa ndege maalum na itacheza mchezo wake na Madagascar Tarehe 14 Novemba, 2021. Licha ya kupoteza mchezo wao jana dhidi ya DR Congo, wameahidi kufanya vizuri dhidi ya Madagascar ili kuibakiza Tanzania kwenye viwango vya juu vya *FIFA*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niungane na wapenda michezo na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuipa pongezi *Taifa Stars* kwa mafanikio makubwa waliyoyapata licha ya kupoteza mchezo wa jana dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Wanasema kuvunjika kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi, hivyo basi hatuna budi kuganga yajayo. Uongozi wa *TFF*, benchi la ufundi la *Taifa Stars* na wadau wote wa soka tutumie matokeo ya jana kujitathmini na kuja na mkakati bora wa kufanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo. Tuendelee kuwekeza kwa vijana wetu, tuboreshe ligi yetu na tuimarishe vilabu vyetu ili tuweze kupata wa chezaji bora watakaoweza kuunda timu ya Taifa kushindana na wenzenzu katika medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Watanzania kwa kufanya mabadiliko ya mfumo wa maisha ya kupenda mazoezi ya viungo yanayofanywa kila pembe sasa hivi nchini kote ikiwemo na kushiriki marathon, *jogging*, mazoezi ya kutembea lakini pia nyumba maalum za mazoezi *Gym*. Napongeza sana wadhamini mbalimbali walioamua kudhamini Timu za Taifa, Vilabu, Makundi ya Mazoezi, Taasisi zilizoanzisha Vikundi vya Michezo, Sanaa na Utamaduni. Tunaanza kuona kuzuri tunakoelekea kuwa na Taifa la wenyе afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuipongeza timu yetu ya Taifa ya Twiga Stars ya Wanawake kwa kuwapa viwanja

vya kujenga nyumba wachezaji wote na walimu wao hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami niungane nawe kuitakia kila kheri Timu yetu ya Bunge Sport kwenye michezo ijayo ya Afrika Mashariki ili ipate ushindi mnono ikiwemo timu yetu ya Wavuta Kamba ambayo ina wavuta Kamba maarufu kwenye Bunge hili (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru tena wote waliosaidia kufanikisha Mkutano tunaoumaliza leo, shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri unayofanya, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri katika kipindi chote cha Mkutano huu wa Tano.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninamshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha Mkutano huu, nawashukuru wale wote waliokuwa na jukumu la ulinzi na usalama ili kuhakikisha Mkutano huu unafanyika na kumalizika salama. Napenda pia niwashukuru madereva wote ambao wametuleta hapa na ambao watafanya kazi nzuri ya kulturudisha makwetu kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa kabisa. Pia ninawashukuru Waandishi wa Habari kwa kuhakikisha kuwa habari za hapa Bungeni zinawafikia wananchi kwa namna mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwashukuru wananchi wa Dodoma na hasa wa Manispaa ya Dodoma kwa ukarimu wao wa kutupatia huduma zote muhimu na hivyo kutuwezesha kukamilisha Mkutano huu kwa mafanikio makubwa na nitumie nafasi hii sasa kuwatakia wote safari njema wakati mnarejea katika maeneo yenu ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunaelekea mwishoni mwa mwaka na Mkutano ujao wa Bunge utakuwa mwakani, naomba nitumie fursa hii kuwatakia Watanzania wote sikukuu njema ya Krismasi na heri ya Mwaka Mpya 2022, tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atuvushe sote na atufikishe

salama mwaka 2022 ili tuweze kukutana tena katika Mkutano wa Sita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya yote, naomba sasa kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, Februari Mosi, 2022 litakapokutana tena Saa Tatu Asubuhi hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MHE. KASSIM M. MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU
WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI
AKIAHIRISHA MKUTANO WA 5 WA BUNGE LA 12 LA JAMHURI
YA MUUNGANO WA TANZANIA, TAREHE 12 NOVEMBA, 2021
JIJINI DODOMA- KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

Shukrani

1. *Mheshimiwa Spika*, leo tunafikia tamati ya mkutano wa tano wa Bunge lako tukufu ulioanza tarehe 2 Novemba, 2021. Kwa msingi huo, tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye mkutano huu tukiwa buheri wa afya.

2. *Mheshimiwa Spika*, ni dhahiri kuwa weledi, busara na uwezo mkubwa uliouonesha katika kuliongoza Bunge hili umekuwa chachu ya kuhitimisha shughuli za Bunge hili kwa mafanikio makubwa. Hivyo basi, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitokushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa.

3. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, niwashukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kukusaidia kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu tukufu.

4. *Mheshimiwa Spika*, ninawashukuru pia, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi nzuri, michango, maoni na ushauri tulioupokea katika mukutano huu. Serikali kwa upande wake imepokea michango yenu yenze nia ya kujenga na kuimarisha utendaji wa Serikali na inaahidi kuifanyia kazi.

Salamu za Pole

5. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 27 Septemba 2021, Bunge lako tukufu lilipata pigo kubwa kwa kuondokewa na Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji). Ninatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Ngorongoro, ndugu, jamaa na marafiki wote walioguswa na msiba huo.

6. *Mheshimiwa Spika*, halikadhalika, katika kipindi hicho cha Septemba hadi Novemba 2021, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na masahibu mbalimbali ikiwemo ajali za barabarani ambazo zimegharimu maisha ya watu, majeruhi na kusababisha uharibifu wa mali. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema na awaponye majeruhi wote. **Amin!**

Salamu za Pongezi

7. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 12 Septemba, 2021 vilevile, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri ambapo alimteua Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb.) kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb.) kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa January Yusuf Makamba (Mb.) kuwa Waziri wa Nishati; Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

8. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwatakitia heri katika kutimiza majukumu yao viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali. Niwakumbushe tu kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania anayo matarajio makubwa kutoka kwenu katika kutimiza shauku ya Watanzania kuona mafanikio kwenye sekta mnazozisimamia.

SHUGHULI ZA BUNGE

Maswali na Majibu

9. Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu jumla ya maswali **98** ya msingi na mengine **247** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali **nane** ya papo kwa papo yalelekezwa kwa Waziri Mkuu na kujibiwa.

Taarifa za Kamati

10. Mheshimiwa Spika, Bunge lilipokea na kujadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye mkutano wa tatu, tarehe 9 Aprili, 2021 na mkutano wa nne, tarehe 7 Septemba, 2021 pamoja na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

Miswada ya Sheria

11. Mheshimiwa Spika, tunapohitimisha mkutano huu, tumeweza kukamilisha mjadala wa miswada miwili ya sheria iliyowasilishwa katika Bunge lako tukufu. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2021 ulisomwa kwa hatua zake zote na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 7 wa Mwaka 2021 ulisomwa kwa mara ya kwanza.

12. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika mkutano wa 4 wa Bunge la 12, Serikali iliahidi kuwasilisha Muswada wa Sheria kuhusu Bima ya Afya kwa Wote. Serikali inatoa umuhimu mkubwa kwenye suala hili sambamba na kuhakikisha masuala yote ya kisera, kisheria na kibajeti yanatazamwa kwa kina. Hatua muhimu za awali zimekamilika na sasa tunawashirikisha wadau wengi zaidi ili kutengeneza mfumo ambaa hautokuwa na changamoto nyingi.

13. *Mheshimiwa Spika*, lengo la Serikali ni kuona utekelezaji wake unaanza mwaka ujao wa fedha 2022/2023 ili kila mwananchi awe na uhakika wa kupata matibabu kila itakapolazimu. Hivyo basi, nitoe maelekezo kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ishirikiane na wadau wote muhimu katika kuhakikisha Muswada wa Sheria kuhusu Bima ya Afya kwa Wote unakamilika kwa wakati ili kukidhi malengo ya Serikali na matarajio ya wananchi.

MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19

14. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 10 Oktoba 2021, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO-19 jijini Dodoma.

15. *Mheshimiwa Spika*, mpango huo uliotokana na mkopo nafuu wa takriban shilingi trillioni 1.3 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) unaolenga kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukabiliana na athari za UVICO19 katika uchumi na maisha ya Watanzania kwa ujumla.

16. *Mheshimiwa Spika*, sekta zitakazonufaika na mpango huo ni Maji (shilingi bilioni 139.4), Elimu (shilingi bilioni 368.9), Afya (shilingi bilioni 466.9), Utalii (shilingi bilioni 90.2), Jamii inayoishi kwenye mazingira magumu (shilingi bilioni 5.5) zikiwemo kaya maskini na Kundi la Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu (shilingi bilioni 5). Aidha, shilingi bilioni 231 zimeelekezwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi bilioni 5 ni kwa ajili ya shughuli za uratibu.

17. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa mpango huo utaimarisha miundombinu ya afya, elimu, maji, utalii, maeneo ya biashara za wajasiriamali wadogo, uwezeshaji wa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na kaya masikini. Kwa upande mwingine, mpango huo utaimarisha upatikanaji sambamba na kusogea huduma za jamii karibu na wananchi. Hii inatokana na ukweli kwamba uwekezaji mkubwa umefanywa kwenye eneo la vifaa

hususan mitambo ya uchimbaji wa maji na visima na vifaa tiba.

18. *Mheshimiwa Spika*, fedha hizo za dharura zinapaswa kutumika ndani ya kipindi cha miezi tisa hususan mwaka huu wa fedha 2021/2022. Kwa kuzingatia hilo, Serikali tayari imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha matarajio ya Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa mpango huo yanafikiwa. Baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo: -

Moja: Kuunda kamati za uratibu kwa ngazi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa kila mkoa na Halmashauri ambapo kamati hizi zimejumuisha viongozi kutoka ngazi ya Wizara, Wakuu wa Idara na Vitengo watakaokuwa na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa miradi yote ilioainishwa;

Mbili: Kuandaa utaratibu wa manunuvi ya pamoja kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa vifaa vyta huduma za dharura, ICU, X-Ray, magari ya kubebea wagonjwa ambayo yatagawiwa katika Halmashauri zote na Magari ya uratibu wa huduma za afya katika Mikoa yote;

Tatu: Kuwaelekeza Wakuu wote wa Mikoa, Wilaya na Watendaji wa Halmashauri kuepuka safari zisizo za lazima katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19; na

Nne: Kuhamasisha wananchi na wawakilishi wao kushiriki ipasavyo katika ujenzi wa miradi inayoendelea kwenye maeneo yao na kutoa taarifa endapo watabaini uwepo wa viashiria vyta ubadhirifu wa fedha au vifaa vyta miradi.

19. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na hatua hizo na katika kuhakikisha uwepo wa thamani ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo, ninaelekeza masuala yafuatayo kwa wote wanaohusika: -

Mosi: Viongozi na Watendaji wasimamie na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi yote ilioainishwa kwenye

Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19;

Pili: Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wahakikishe hadi kufikia Januari 2022, madarasa yote kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza yawe yamekamilika;

Tatu: Wakuu wa Mikoa wahakikishe wanasimamia ipasavyo mipango ya usimamizi kuitia Sekretarieti za Mikoa. Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa zihakikishe zinafuatilia utekelezaji huo sambamba na kutembelea maeneo husika ili kujiridhisha na thamani ya fedha zilizotolewa na ujenzi uliofanyika; na

Nne: Wakuu wa Mikoa wahakikishe Sekretarieti husika zinawashirikisha wananchi na wawakilishi wao katika kutekeleza miradi iliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19.

20. *Mheshimiwa Spika*, natambua kwamba ilikuwepo hofu kuhusu kupatikana na wakati mwingine kupanda kwa bei ya baadhi ya vifaa vya ujenzi ikiwemo saruji, bati, nondo, marumaru, vifaa vya umeme n.k.

21. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua ya kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilikutana na wazalishaji na hata kutembelea baadhi ya maeneo ya uzalishaji ili kujiridhisha na hali ilivyo kwa upande wa bidhaa hiso. Nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba wazalishaji wetu wamejipanga vizuri kiuzalishaji na hatutarajji uhaba au mtikisiko wa bei kwa bidhaa lengwa. Niendelee kusisitiza kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara isimamie na ifuatilie mwenendo wa bei ya bidhaa hiso kutoka viwandani hadi kwa walaji.

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2022/2023

22. *Mheshimiwa Spika*, Bunge lako tukufu lilipokea, kujadili, kushauri na kuitisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

23. *Mheshimiwa Spika*, katika kukidhi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3)(c) na Kanuni za Kudumu za Bunge lako tukufu Ibara ya 11, hoja hiyo ilijadiliwa kwa siku tano kuanzia tarehe 3 Novemba 2021 na kuhitimishwa tarehe 09 Novemba 2021.

24. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa maelezo mazuri ya ufanuzi walijotoa wakati wa kuhitimisha hoja hiyo.

25. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa mchango mzuri waliota wakati wa mjadala wa hoja hiyo. Katika mjadala huo, tulipata darasa zuri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wametupa uelewa mpana utakaotusaidia kuboresha utekelezaji wa mpango huo kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu.

26. *Mheshimiwa Spika*, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 ni wa kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

27. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/2023, mpango huo utaendelea kutekeleza maeneo mahsus ya kipaumbele ambayo ni: (i) kuchochlea uchumi shindani na shirkishi; (ii) kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; (iii) kukuza biashara na uwekezaji; (iv) kuchochlea maendeleo ya watu na (v) kuendeleza rasilimali watu.

28. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na mapendekezo ya mpango huo, pia, uliwasilishwa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023. Hivyo, nami nitumie fursa hii kusitiza baadhi ya mambo muhimu ambayo hayanabudi kuzingatiwa kikamilifu na viongozi na watendaji wote wakati wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 kama ifuatavyo:-

Moja: Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani. Hili ni miongoni mwa maeneo yaliyoibua hoja kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Hivyo, nisisitize kuwa Wizara ya Fedha ishirikiane na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuimarisha matumizi ya vifaa vya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali;

Mbili: Riba kubwa za mikopo kutoka kwenye mabenki ya biashara na taasisi za fedha: Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti kupitia Benki Kuu ya Tanzania ikiwemo kupunguza kiwango cha akiba kinachowekwa na mabenki katika Benki Kuu, kulegeza masharti ya uanzishwaji wa ofisi za wakala wa mabenki, kushusha riba inayolipwa kwa akaunti za fedha za mitandao pamoja na kutenga **shilingi trilioni moja** kwa ajili ya mikopo kwa mabenki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia tatu ili mabenki na taasisi hizo zitoe mikopo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zinalenga kupunguza kiwango cha riba kwenye mikopo ya mabenki ya kibiashara na taasisi za fedha, kupunguza riba katika shughuli za kilimo kwa kiwango kisichozi idha asilimia 10 na kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi ili kuchechemua shughuli za kiuchumi. Licha ya hatua hizo, bado kumekuwa na changamoto ya kutoshuka kwa kiwango cha riba kinachotozwa na mabenki na taasisi za fedha. Kwa mantiki hiyo, ninaiagiza Wizara ya Fedha na Mipango ikutane na taasisi za fedha nchini kuona namna wanavyoweza kupunguza riba kubwa kwenye mikopo wanayotoa hususan kwa makundi ya wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo;

Tatu: Kuwawezesha Wakandarasi wa Ndani: Wizara ya Fedha shirikianeni na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika

kuhakikisha inatekeleza vema Mpango wa Serikali wa kuwajengea uwezo na kuwawezesha wakandarasi wa ndani sanjari na kuendelea kulipa madeni ya wazabuni kwa wakati;

Nne: Mafao ya Wastaifu. Katika hili namuelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu) ashirikiane na Waziri wa Fedha na Mipango kuhakikisha changamoto ya upatikanaji wa mafao ya wastaifu kwa wakati inaondoka na wastaifu walipwe kwa wakati;

Tano: Kudhibiti Matumizi na Kupunguza Gharama: Maafisa Masuuli endeleeni kuchukua hatua za kupunguza matumizi ya Serikali yasiyokuwa ya lazima na kuhakikisha kuwa taasisi za Serikali zinazojiendesha kibiashara, zinapata faida na kuacha kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu; na

Sita: Kudhibiti Ongezeko la Madeni ya Serikali: Maafisa Masuuli wote hakikisheni madai ya watoa huduma yote yanahakikiwa na kuingizwa kwenye hesabu za fungu husika, kutoingia mikataba ya miradi mipya bila kuwa na uhakika wa upatikanaji fedha; na kuzingatia matumizi ya hati za ununuzi zinazotolewa kwenye mfumo wa malipo ili kudhibiti ulimbikizaji wa madeni.

29. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha viongozi na watendaji wote Serikalini kuzingatia kikamilifu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023 ili kuendeleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

KILIMO

Utabiri wa Hali ya Hewa na Uhakika wa Chakula Nchini

30. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2020/2021 ulikuwa mzuri. Katika msimu huo uzalishaji ulifikia tani milioni 18.42 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 14.79. Kwa lugha nyingine tuna ziada ya tani milioni 3.63.

31. *Mheshimiwa Spika*, hivi sasa tupo katika msimu wa kilimo 2021/2022 ambapo baadhi ya maeneo ya nchi yetu yameanza kupata mvua za vuli. Hata hivyo, taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania iliyotolewa Septemba na Oktoba 2021 imeonesha kuwa viwango vya unyeshaji mvua katika msimu huu wa kilimo vitakuwa vya wastani katika baadhi ya maeneo hali imbayo itaathiri uzalishaji wa baadhi ya mazao kama mpunga na mahindi kutokana na vipindi virefu vya ukame.

32. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeshachukua hatua mahsusili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na upungufu wa mvua. Hatua hizo ni pamoja na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuendelea kununua chakula na kuhifadhi na kufuatilia kwa karibu mwenendo wa ukuaji wa mazao shambani sambamba na kufanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu 2021/2022.

Hali ya Upatikanaji wa Mbolea

33. *Mheshimiwa Spika*, ni dhahiri kuwa matumizi ya mbolea, mbegu bora na viuatilifu ni muhimu katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika kuzalisha, kuagiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima kulingana na mahitaji na ikolojia ya kilimo. Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa katika kuhakikisha pembejeo za kilimo hususan mbolea zinapatikana kwa bei nafuu, kwa wakati lakini pia kwa kiwango cha kutosha. Miongoni mwa hatua hizo ni matumizi ya mifumo ya upatikanaji wa mbolea kuitia uzalishaji ndani ya nchi na uagizaji wa mbolea kwa pamoja kutoka nje ya nchi.

34. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa 2021/2022 makisio yanaonesha kuwa mahitaji ya mbolea ni tani 698,260 na wastani wa matumizi kwa mwaka ni tani 430,000. Hata hivyo, hadi kufikia Oktoba 2021 upatikanaji wa mbolea ulikuwa ni tani 333,903 sawa na asilimia 48 ya mahitaji.

35. *Mheshimiwa Spika*, hali ya upatikanaji wa mbolea duniani kote imeathiriwa na uwepo wa UVIKO 19. Hali hiyo, imesababisha kusimama kwa uzalishaji, baadhi ya nchi

kusitisha uuzaaji wa mbolea nje, kuongezeka kwa ghamama za usafirishaji na upungufu wa malighafi za kutengeneza mbolea kutokana na baadhi ya nchi kufunga mipaka yake na hivyo kusababisha ongezeko la mahitaji na bei ya mbolea.

36. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na kusuasua kwa uagizaji wa mbolea na ongezeko la bei kwa takribani asilimia 96 ikilinganishwa na bei ya mwaka jana, Serikali imechukua hatua za haraka kukabiliana na hali hiyo kama ifuatavyo:-

Moja: Kuwasiliana moja kwa moja na wazalishaji wa mbolea katika nchi rafiki ili kupata mbolea kwa ghamama nafuu;

Mbili: Kuruhusu wafanyabiashara kuingiza mbolea nchini bila kutumia zabuni za mfumo wa ununuzi wa pamoja na kuuza kwa bei ya ushindani. Hatua hii imesaidia kuongeza kiwango cha mbolea kilichoingizwa nchini kati ya Julai na Oktoba 2021. Katika kipindi hicho, tani 48,400 za mbolea ya urea ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 33,948 zilinunuliwa kwa zabuni ya mfumo wa pamoja msimu wa 2020/2021;

Tatu: Kuhamasisha matumizi ya mbolea mbadala wa DAP na Urea kama vile NPK, NPS, NPSZinc, Nafaka+ ya Minjingu, mbolea za asili, chokaa na mbolea ya Fomi Imbura inayozalishwa na Kiwanda cha Fomi cha Burundi;

Nne: Kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea ikiwa ni sehemu ya suluhisho la muda mrefu. Tayari ujenzi wa kiwanda cha Kampuni ya Itracom Fertilizers Limited kutoka Burundi umeanza na utakapokamilika kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka. Kadhalika, kuongeza uzalishaji katika kiwanda cha Minjingu ili kizalishe sawa na uwezo wake wa tani 100,000 kwa mwaka;

Tano: Kukamilisha mazungumzo na Serikali ya Burundi kuhusu kununua mbolea ya Fomi Imbura. Nitoe wito kwa Watanzania kuzitumia aina nyingine za mbolea kwani zinatumika kwa mafanikio kwa nchi jirani na hata baadhi ya maeneo ya Tanzania;

Sita: Serikali kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) imekwishaagiza tani 20,000 za mbolea ya kupandia (DAP) na tani 60,000 za mbolea ya kukuzia (Urea). Mbolea hii itauzwa kwa gharama nafuu ambayo inalingana na uwezo wa wakulima wetu nchini; na

Saba: Kukamilisha utafiti wa afya ya udongo katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Tanga, Ruvuma, Tabora na Kigoma kwa lengo la kuwezesha viwanda nya mbolea hususan vilivyo nchini kuzalisha mbolea kulingana na afya ya udongo sambamba na matumizi sahihi ya mbolea.

37. *Mheshimiwa Spika*, Serikali itaendelea kutoa taarifa muhimu na elimu kwa umma kuhusu hali ya hewa na bei ya mbolea duniani. Niwaagize Wakuu wa Mikoa hasa ya mipakani wasizue mbolea kuingizwa nchini kwa sababu bado uhitaji ni mkubwa na pia wasiruhusu mbolea iuzwe nje ya nchi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnaporudi kwenye majimbo yenu mtoe elimu kwa wananchi kuhusu changamoto ya bei ya mbolea na kuhamasisha matumizi ya mbolea mbadala zinazopatikana kwa bei nafuu.

UMWAGILIAJI

38. *Mheshimiwa Spika*, kwa sasa Taifa letu lina mfumo wa umwagiliaji wenyewe ukubwa wa hekta 600,000 ambao mtandao huo pamoja na uwepo wake haufanyi kazi kwa asilimia 100. Kwa kuzingatia llani ya Uchaguzi ya CCM; lengo la Serikali ni kuhakikisha sekta ya umwagiliaji inakuwa na miundombinu ya umwagiliaji yenyewe ukubwa wa hekta milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025.

Ninawaagiza Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha kukaa pamoja na kufanya mambo yafuatayo kwenye mpango wa 2022/23 na bajeti ya mwaka ujao wa fedha:-

(1) Kuhakikisha kila Mkoa na Wilaya kuna Ofisi ya Tume ya Umwagiliaji na vitendea kazi na wahandisi wenyewe sifa.

- (2) Kuhakikisha wahandisi wa umwagiliaji waliopo kwenye Halmashauri na wahandisi wa Tume ya Umwagiliaji wanafanya kazi chini ya Ofisi za Tume ya Umwagiliaji.
- (3) Kufanya usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji kwa maeneo mapya ili kujenga skimu mpya zenye ukubwa wa hekta 600,000 kufikia mwaka 2025.
- (4) Kufanya tathmini ya kina yaskimu za umwagiliaji zilizopo na kuzikarabati ili ziweze kufikia ubora na ufanisi unaotakiwa.
- (5) Kutenga fedha kupitia bajeti ya Wizara kwa ajili ya kununua vifaa na mitambo ambayo itakuwa katika kanda nane za kilimo ili zitumike kutunza, kurekebisha na kujenga mabwawa madogo madogo kwenye maeneo ambayo wakati wa masika maji mengi hupotea.
- (6) Wizara ya Fedha kwa pamoja na Wizara ya Kilimo andaeni miradi ya kielelezo ya umwagiliaji, maghala na uwekezaji kwenye maeneo ya uhifadhi wa mazao ya nafaka na mazao ya bustani (Horticulture).

UMEME VIJJINI

39. *Mheshimiwa Spika*, mionganoni mwa hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mkutano huu ni pamoja na suala la kuharakisha upatikanaji wa umeme vijiji. Kama alivyoeleza Waziri wa Fedha na Mipango alipokuwa akiwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme hususan maeneo ya vijiji.

40. *Mheshimiwa Spika*, hadi sasa jumla ya vijiji 10,361 kati ya vijiji 12,317 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 84.12 vimeunganishiwa umeme. Lengo la Serikali ni kuhakikisha hadi kufikia Desemba 2022 vijiji 1,956 vilivyosalia vinapata umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vijiji Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulioanza kutekelezwa Julai, mwaka huu. Gharama za mradi huu ni shilingi triliuni 1.24.

41. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha maeneo yote ya mijini na vijiji yanapata umeme wa kutosha, nafuu na uhakika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji na usambazaji umeme maeneo mbalimbali nchini. Baadhi ya miradi ya kimkakati ya uzalishaji umeme ni mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (MW 2,115) ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 55.6 na mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo (MW 80) uliofikia asilimia 81.2.

42. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Serikali imekamilisha mradi wa njia ya kusafirisha umeme (KV 220) kutoka Bulyanhulu hadi Geita wenye urefu wa kilomita 55. Miradi mingine ya kusafirisha umeme inayoendelea kutekelezwa ni kutoka Rusumo kwenda Nyakanazi kupitia Benaco (KV220), Tabora kupitia Urambo - Nguruka hadi Kidahwe (KV 132) na Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga (KV132). Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa KV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga na mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa KV 400 kutoka Sumbawanga – Mpanda hadi Kigoma.

43. *Mheshimiwa Spika*, kukamilika kwa mraidi hiyo ya uzalishaji na usambazaji umeme kutawezesha maeneo yote nchini kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa na hivyo kupata huduma ya uhakika ya umeme. Jukumu la TANESCO ni kuhakikisha usambazaji umeme kwenye makazi ya watu unafanywa kwa kasi ili lengo la Mheshimiwa Rais la kuona kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme liweze kutimia.

MIKOPO YA ELIMU YA JUU

44. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu kwa kuongeza kiwango cha fedha za kugharamia mikopo ya elimu ya juu na hivyo kuongeza idadi ya wanufaika. Kwa mfano, katika mwaka wa masomo 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu ikililinganishwa na shilingi bilioni 464 zilizotumika mwaka 2020/2021. Vilevile, idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka 149,398 mwaka 2020/2021 hadi 170,000 mwaka 2021/2022.

45. *Mheshimiwa Spika*, upangaji wa mikopo unaendelea kwa kuzingatia utaratibu, sifa na vigezo vilivyowekwa. Kwa msingi huo, ninaelekeza kama ifuatavyo: -

Moja: Waombaji wote wa mikopo hakikisheni mnakamilisha taratibu za uombaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kujisajili kwenye mfumo wa maombi ya mikopo (OLAMS) kwa wakati. Vilevile, hakikisheni mnawasilisha taarifa sahihi ili muweze kuhudumiwa bila bughudha;

Mbili: Baada ya kufunguliwa kwa dirisha la rufaa, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu harakisheni mchakato wa rufaa ili wanafunzi husika waweze kupata stahiki zao, watulie na kuendelea na masomo yao kama kawaida;

Tatu: Mamlaka zote za vyuo vikuu vyenye wanafunzi wanaonufalka na mikopo ya elimu ya juu kamillisheni na kuwasilisha taarifa za wanafunzi ili kuiwezesha Bodi ya Mikopo kuwapangia mikopo na kuhakikisha wanapokea stahili zao kwa wakati na kupunguza usumbufu usiokuwa wa lazima.

46. *Mheshimiwa Spika*, licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utoaji mikopo ya elimu ya juu, Serikali imepokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuboreshwa kwa mfumo wa sasa wa mikopo ya elimu ya juu. Maoni hayo ni pamoja kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya katii.

47. *Mheshimiwa Spika*, maoni mengine ni kutoa ruzuku badala mikopo kwa wanafunzi wanaosomea shahada na stahashada zenye uhitaji mkubwa kitaifa na katika uzalishaji, na wale wanaotoka katika makundi yenye mahitaji maalum; lakini pia kufanya mapitio ya vipengele vya mikopo ili kuangalia uwezekano wa kuainisha vipengele vya kukopeshwa na vinavyoweza kutolewa kama ruzuku kati ya gherama za ada za mafunzo na zile za mahitaji mengineyo.

48. *Mheshimiwa Spika*, ninaelekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya upya mapitio ya mfumo wa utoaji

mikopo ili kuzingatia maoni ya wadau na uzoefu wa miaka iliyopita na ije na mapendekezo kuhusu mfumo bora utakaotatua changamoto za sasa sambamba na kuimarisha kasi ya urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu.

BANDARI

49. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kufanya maboresho makubwa ya bandari zetu zilizopo kwenye Bahari ya Hindi na maziwa makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Maboresho hayo, yanalenga kuongeza uwezo wa bandari zetu katika kuhudumia meli hususan za shehena na hivyo, kumudu ushindani wa kibiashara sambamba na kutumia vema fursa ya kijirografia katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Bandari ya Dar es Salaam

50. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 421 umefikia asilimia 99 na unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2021/2022. Kukamilika kwa mradi huu, kutaongeza uwezo wa bandari ya Dar es Salaam wa kuhudumia meli kubwa zinazohitaji kina kirefu zaidi kuliko ilivyo sasa, zenye urefu wa hadi mita 305 na uwezo wa kubeba makasha kati ya 7,000 hadi 8,000.

51. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, uwezo wa bandari hiyo wa kuhudumia shehena kubwa ya mizigo utaongezeka kutoka tani milioni 16 za sasa hadi tani milioni 25. Hivyo, kuongeza mapato ya Taifa na kumudu ushindani na bandari nyingine za ukanda wa Bahari ya Hindi kama vile Mombasa, Maputo, Beira, Nacala na Durban.

52. *Mheshimiwa Spika*, hivi sasa bandari ya Dar es Salaam imeanza kupokea meli kubwa zenye uwezo wa kubeba hadi magari 6,000 pamoja na kuongeza uwezo wa kuhudumia meli kubwa hadi tatu za aina moja ya shehena kwa wakati mmoja.

Bandari ya Tanga

53. *Mheshimiwa Spika*, awamu ya kwanza ya uboreshaji wa Bandari ya Tanga ambayo ilihuisha uongezaji wa kina cha

lango la bandari kutoka mita 4 hadi mita 13 na ujenzi wa gati mbili kwenye kina kirefu umekamilika. Katika mwaka 2020/2021, mradi huo uligharimu shilingi bilioni 20.41.

54. *Mheshimiwa Spika*, awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari hiyo wenyewe lengo la kuongeza kina cha gati utekelezaji wake umefikia asilimia 13. Kukamilika kwa mradi huo, kutaiwezesha bandari ya Tanga kuondokana na gharama kubwa za kuhudumia meli nangani.

Bandari ya Mtwara

55. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa bandari ya Mtwara, awamu ya kwanza ya ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 litakalohudumia shehena mchanganyiko umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, ukarabati wa yadi ya kuhudumia shehena kupitia ujenzi wa sakafu ngumu eneo la mita za mraba 5,600 na ukarabati wa ghala namba 3 nao umekamilika.

56. *Mheshimiwa Spika*, maboresho hayo yanayoendelea yana lengo la kuhakikisha Bandari ya Mtwara inakuwa endelelevu kwa kusafirisha bidhaa na mazao yanayozalishwa mikoa ya Kusini ikiwemo zao kuu la korosho na mazao mengine kama ufuta na makaa ya mawe kutoka Ngaka. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeongeza uwezo wa Bandari ya Mtwara kuhudumia shehena ambapo kwa sasa ina uwezo wa kuhudumia tani 1,000,000 kwa mwaka ikilinganishwa na tani 400,000 za awali.

57. *Mheshimiwa Spika*, upanuzi wa bandari ya Mtwara umeongeza uwezo wake na kuifanya iweze kuhudumia meli nne kwa wakati mmoja. Vilevile, maeneo ya wazi ya kuhudumia na kuhifadhi shehena yaliyosakafiwa yameongezwa hadi kufikia uwezo wa kuhudumia makasha 12,950 kwa wakati mmoja. Hali kadhalika, maghala ya kuhifadhi mizigo yaliyopo yana uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 kwa wakati mmoja.

58. *Mheshimiwa Spika*, hatua nyingine zinazokwenda sambamba na maboresho hayo ni kupungua kwa tozo ya aridhia kwa mazao ya kilimo kutoka asilimia moja hadi asilimia 0.5 ya mali pwani ikilinganishwa na bandari nyingine nchini. Vilevile, kuongeza muda wa makasha tupu kukaa bandarini kutoka siku 15 na kuwa muda wa kipindi chote cha msimu wa korosho na kuongeza muda wa makasha yenye mzigo kukaa bandarini bila tozo ya kuhifadhi kutoka siku saba hadi siku 15 na kupunguza ya tozo za kuhudumia meli na shehena kwa asilimia 30.

59. *Mheshimiwa Spika*, maboresho yanayoendelea katika bandari ya Mtwara ikiwemo kuweka unafuu wa gharama za kuhudumia shehena yanalenga kuongeza matumizi ya bandari hiyo hususan katika usafirishaji wa mazao ya kilimo, jasi (gypsum), makaa ya mawe kutoka Ruvuma sambamba na kuku shughuli za kiuchumi katika ushoroba wa Mtwara.

Bandari za Maziwa Makuu

60. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kwa upande mwingine imeendelea na uboreshaji wa bandari zilizopo kwenye maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ili ziweze kutoa huduma bora na kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo.

61. *Mheshimiwa Spika*, uboreshaji wa bandari mbalimbali katika Ziwa Victoria kuititia ujenzi wa gati, majengo ya utawala na abiria na maghala ya kuhifadhi mizigo katika bandari za Magarine (Muleba), Nyamirembe (Chato), Bukoba, Kemondo Bay, pamoja na ujenzi wa gati mbili katika bandari ya Mwigombero (Musoma) na gati moja katika bandari za Lushamba na Nkome umekamilika.

62. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Ziwa Tanganyika, Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Kibirizi na Ujiji umekamilika kwa asilimia 52 na ujenzi wa bandari ya Karema umekamilika kwa asilimia 55. Aidha, ujenzi wa miundombinu mingine ikiwemo majengo ya abiria na ghalia la kuhifadhia mizigo katika bandari za Kasanga, Sibwesa, Kabwe, Kipiri na Lagosa (Mpanda Vijijini), Kabwe (Nkasi) na Ujiji unaendelea.

63. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ziwa Nyasa, ujenzi wa bandari na miundombinu mingine ikiwemo majengo ya abiria na ghala la kuhifadhiya mizigo katika bandari ya Ndumbi umefikia asilimia 82.

64. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kuboresha miundombinu na utoaji huduma za bandari ili kuongeza chachu ya maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Hivyo basi, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kuendelea kumuunga Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na dhamira yake ya dhati ya kutuletea maendeleo.

UTAMADUNI, SANAANNA NA MICHEZO

65. Mheshimiwa Spika, Taifa letu linaendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika fani za utamaduni, sanaa na michezo. Shughuli mbalimbali za utamaduni, sanaa na michezo zimeendelea kuling'arisha Taifa letu kwa viwango tofauti ndani na nje ya nchi.

66. Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu unatangazwa vyema kupitia shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo matamasha ya ngoma, mavazi, vyakula vyaa makabila mbalimbali n.k. Hivi karibuni Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo kiliendesha Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania na lilipata mafanikio makubwa na mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia pia taasisi ya Tulia Foundation ya Mbeya, hivi karibuni iliandaa tamasha la ngoma za Utamaduni ambalo lilitfana sana.

67. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sanaa yapo maendeleo makubwa ikiwemo kuhusisha wasanii wengi ambaao hujipatia kipato kupitia fani hiyo. Muziki wa aina zote, uchoraji, uchongaji na maendeleo ya filamu yamekuwa chachu ya kukua kwa sanaa yetu nchini. Hivi karibuni tulitembelewa na Msanii maarufu wa filamu Sanjay Dutt kutoka India kwa lengo la kuja kuanzisha ushirikiano na wasanii wa filamu wa Tanzania na India. Pia kutangaza utalii

wetu. Bado yuko mbugani ambako anakagua maeneo ya kupiga picha na kutengeneza filamu ya mbunga zetu ili kulitangaza Taifa letu.

68. *Mheshimiwa Spika*, kwenye michezo nako yako mafanikio makubwa yamefikiwa ambako michezo mbalimbali inaendelea kuchezwa. Timu za mpira wa miguu na mpira wa kikapu ziko kwenye Mashindano ya Kombe la Taifa chini ya udhamini wa CRDB kwenye michuano inayoendelea viwanja vya Chinangali hapa Dodoma, Timu za Taifa za Mpira wa Miguu kutoka mikoa mbalimbali zinaendelea na mashindano kwa ngazi mbalimbali. Kwa upande wa soka, timu zetu zimekuwa zikifanya vizuri. Ninawapongeza Twiga Stars kwa kufanikiwa kubeba kombe la COSAFA katika fainali zilizofanyika Afrika Kusini baada ya kuzifunga Afrika ya Kusini, Zimbabwe, Botswana, Sudani, Zambia na Malawi, na kutoa mchezaji bora wa mashindano hayo ambaye ni Amina Bilali.

69. *Mheshimiwa Spika*, timu yetu ya Wanawake ya Chini ya Miaka 20 “Under 20”, imefuzu hatua ya tatu ya kucheza Kombe la Dunia bado hatua mbili ambazo wakishinda watacheza Kombe la Dunia. Timu hii imeshika nafasi ya tatu katika mashindano ya CECAFA Under 20. Mchezaji wetu Aisha Masaka alipata tuzo ufungaji bora kwa kufunga magoli saba kwenye michezo mmoja. Timu ya Vijana Under 20, walichukua ubingwa CECAFA Wanaume kwa kuifunga Congo goli moja.

70. *Mheshimiwa Spika*, timu yetu ya Wanaume Taifa Stars inayoendelea na mashindano ya kufuzu hatua za awali za Kombe la Dunia imeondoka leo kwenda Madagascar kwa ndege maalumu na itacheza tarehe 14 Novemba, 2021. Licha ya kupoteza michezo wao jana dhidi ya DR Congo, wameahidi kufanya vizuri dhidi ya Madagascar ili kuibakiza Tanzania kwenye viwango vya juu vya FIFA.

71. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, niungane na wapenda michezo na Watanzania wote kwa ujumla kuipa pongezi Taifa Stars kwa mafanikio makubwa waliyoyapata licha ya

kupoteza mchezo wa jana dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

72. *Mheshiwa Spika*, kuvunjika kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi, hivyo nasi hatuna budi kuganga yajayo. Uongozi wa TFF, benchi la ufundi la Taifa Stars na wadau wote wa soka tutumie matokeo ya jana kujitathmini na kuja na mkakati bora wa kufanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo. Tuendelee kuwekeza kwa vijana wetu, tuboreshe ligi yetu na tuimarishe vilabu vyetu ili tuweze kupata wachezaji bora ambao wanaweza kushindana na wenzetu katika medani za kimataifa.

73. *Mheshimiwa Spika*, nitumie nafasi hii kuwapongeza Watananzania kwa kufanya mabadiliko ya kitabia ya kupenda mazoezi ya viungo yanayofanywa kila pembe nchini kwa kushiriki *marathon, jogging*, mazoezi ya kutembea pia nyumba maalum za mazoezi (*Gym*). Napongeza sana wadhamini mbalimbali walioamua kudhamini timu za taifa, vilabu, makundi ya mazoezi, taasisi zilizoanzisha vikundi vya michezo, sanaa na utamaduni. Tunaanza kuona kuzuri tunakoelekea kuwa na Taifa la watu wenye afya timamu.

74. *Mheshimiwa Spika*, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwapongeza Twiga Stars na kuwapa viwanja vya kujenga nyumba wachezaji na wa alimu wao hapa Dodoma. Nami niungane nawe Mheshimiwa Spika katika kuitakia heri timu yetu ya Bunge itakayoshiriki michuano ya Mabunge ya Afrika Mashariki huko Arusha, na hasa timu yetu ya wavutakamba.

HITIMISHO

75. *Mheshimiwa Spika*, nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru tena wote waliosaidia kufanikisha mukutano tunaoumaliza leo. Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa katuongoza vizuri katika kipindi chote cha mukutano huu wa tano.

76. Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha mukutano huu. Nawashukuru wale wote waliokuwa na jukumu la ulinzi na usalama ili kuhakikisha mukutano huu unafanyika na kumalizika salama. Napenda pia niwashukuru madereva wote kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa. Ninawashukuru pia waandishi wa habari kwa kuhakikisha kuwa habari za hapa Bungeni zinawafikia wananchi kwa namna mbalimbali.

77. Mheshimiwa Spika, mwisho, niwashukuru wananchi wa Dodoma na hasa wa Jiji la Dodoma kwa ukarimu wao wa kutupatia huduma zote muhimu na hivyo kutuwezesha kukamilisha mukutano huu kwa mafanikio makubwa. Nitumie nafasi hii sasa kuwatachia wote safari njema wakati mnarejea katika maeneo yenu ya kazi.

78. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunaelekea mwishoni mwa mwaka na mukutano ujao wa Bunge utakuwa mwakani, naomba nitumie fursa hii kuwatachia Watanzania wote sikuu njema ya Krismasi na heri ya Mwaka Mpya 2022. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atuvushe sote na atufikishe salama mwaka 2022 ili tuweze kukutana tena katika Mkutano wa 6 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

79. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu sasa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 1 Februari, 2022 litakapokutana tena saa 3.00 asubuhi hapa jijini Dodoma.

80. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Hoja imetolewa Waheshimiwa Wabunge na imeungwa mkono sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo imetoa muhtasari wa shughuli ambazo tumezifanya na pia imekuwa na taarifa

nyingi muhimu kwa Taifa letu na Watanzania kwa ujumla.
Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:
Wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

SPIKA: Naomba tusimame kwa wimbo wa Taifa,
kwaya ya Bunge

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki
ziliimbwa na Kwaya ya Bunge)*

SPIKA: Tukiwa bado tumesimama kwanza ahsante
sana Kwaya ya Bunge muendelee kujifua tunatumaini
mtashiriki kwenye shughuli za miaka 60 ya Uhuru ili muwe na
nyimbo za namna hiyo mtunge na mfanyie mazoezi ili katika
shughuli hizo basi tutakutana na kwaya ya Mahakama na
kwaya ya Utumishi Serikalini kwaya yetu iwe bora kuliko zile
zingine zote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tukiwa bado tumesimama
tunapaswa kufanya uamuzi hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu
ya kwamba Bunge liahirishwe hadi tarehe Mosi Februari, 2022.
Wanaoafiki jambo hilo waseme ndiyo.

WABUNGE FULANI: Ndiyo

SPIKA: Wasioafiki waseme siyo.

WABUNGE FULANI: Siyo. (*Kicheko*)

SPIKA: Hawa wanataka wabaki Dodoma mpaka
mwakani hawa. Nadhani walioafiki wameshinda. (*Makofi/*
Kicheko)

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaondoka tunawaombea mwende salama, mfike salama Mungu awatangulieni, Serikali tunawatachia kila la kheri. Tunaondoka jambo moja lipo *pending* kidogo la mbolea, lakini sisi tutakuwa tumeondoka tunaomba tu huku nyuma Serikali mje mtoe kauli thabiti kwa Watanzania kuhusiana na suala la mbolea kwa sababu ni suala kubwa baada ya kuwa mmelifanya kazi vizuri zaidi ili kuwe na uelewa kuhusiana na jambo hilo kwa ujumla wake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, basi niwatakie kila heri, niwaombe sana madereva wetu tuwa-*control* tuendeshe wenyewe, si kwa kushika *starring*, lakini kwa kumuambia punguza *speed maximum 80, maximum 90* sio zaidi ya hapo. Niwatakie kila la heri kwa *Christmas*, kwa mwaka mpya tuombeane heri sote tuione 2022 na Mungu awabariki sana.

WABUNGE FULANI: *Amen. (Makofi)*

SPIKA: Basi sasa tunaahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe aliyoitaja Mheshimiwa Waziri Mkuu mwakani Februari, tarehe Mosi.

*(Saa 10:35 Jioni Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 1 Februari, 2022 Saa Tatoo Asubuhi)*